

## **Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)**

**BUNGE LA TANZANIA**

**MKUTANO WA PILI**

**Kikao cha Nane – Tarehe 18 Februari, 2011**

*(Mkutano Ulianza Saa 3.00 Asubuhi)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Anne S. Makinda) Alisoma Dua*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge tusimame kwa muda wa dakika moja tuwakumbuke Wenzetu, Ndugu zetu, waliopoteza maisha katika matatizo yaliyotokea Gongo la mboto - Jijini Dar es Salaam.

*(Hapa Waheshimiwa Wabunge walismama kwa dakika  
moja kuwakumbuka waliopoteza maisha kwa  
kulipukiwa na mabomu)*

**SPIKA:** Ahsanteni sana Waheshimiwa Wabunge. Wote wapumzike kwa amani huko walikokwenda. Ahsanteni sana, tukae.

**HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI**

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:**

Taarifa ya mwaka na Hesabu za Shirika la Viwango Tanzania (TBS) kwa mwaka 2008/2009 (*The Annual Report and Accounts of Tanzania Bureau of Standards, for the year 2008/2009*).

Taarifa ya mwaka na Hesabu za Shirika la Kuendeleza Viwanda Vidogo (SIDO) kwa mwaka 2008/2009 (*The Annual Report and Accounts of Small Industries Development Organization (SIDO) for the year 2008/2009*).

## **MASWALI NA MAJIBU**

**MHE. TUNDU A. M. LISSU:** Mheshimiwa Spika, mwongozo wa Spika.

**SPIKA:** Sawa.

**MHE. TUNDU A.M. LISSU:** Mheshimiwa Spika, naomba kupata idhini yako Mheshimiwa Spika chini ya Kanuni ya 150(i) inayohusu Kanuni yoyote inaweza kutenguliwa kwa madhumuni mahususi baada ya Waziri, Mwanasheria Mkuu wa Serikali au Mbunge yoyote kutoa hoja kwa ajili hiyo Mheshimiwa Spika na Kanuni ambayo naomba itenguliwe.

**SPIKA:** Sasa mwongozo au kutengua Kanuni. Kuna mambo mawili, mwongozo ni kutaka nikusaidie ufanye nini. Hayo unayotaka kufanya, nini sasa?

**MHE. TUNDU A.M. LISSU:** Naomba Mheshimiwa Spika,

**SPIKA:** Mwongozo au?

**MHE. TUNDU A.M. LISSU:** Naomba kutoa hoja kutengua Kanuni Mheshimiwa Spika, kwa sababu mahususi.

**SPIKA:** Eeeehee eleza sababu zenyewe kwanza.

**MHE. TUNDU A. M. LISSU:** Mheshimiwa Spika, juzi kumetokea milipuko ya mabomu kwenye ghala ya silaha Gongolamboto Dar es Salaam na limeliingiza Taifa katika msiba mkubwa na jambo hili lisisababisha Bunge lako Tukufu liahirishwe jana na leo tumesimama kwa dakika moja kuwakumbuka wale wote waliopoteza maisha. Jambo hili ni kubwa. Naomba kwanza nitoe hoja kwamba Kanuni ya 47 na ya 48 inayohusu kujadili jambo la dharura itenguliwe ili kuruhusu Bunge hili tukufu lijadili hili jambo mahususi la milipuko ya Gongolamboto kwa sababu kanuni zilivyo sasa hivi hili jambo haliwezi likajadiliwa Bungeni hapa bila kwanza kutenguliwa kwa Kanuni. Ahsante Mheshimiwa Spika.

**SPIKA:** Kwani katoa hoja. Hajatoa hoja, huyu ameomba mwongozo wa Spika, kifungu cha 47 ambacho kinazungumzia kuahirisha shughuli za Bunge ili kujadili jambo la dharura, ndiyo kifungu chenyewe hicho.

Sasa hiki kifungu kina maelezo mengi, kwanza kifungu cha kwanza kinasema hivi, “Baada ya muda wa maswali kwisha Mbunge yoyote anaweza kutoa hoja kuwa shughuli za Bunge kama zilivyoonyeshwa kwenye Orodha ya Shughuli zilizoainishwa ili Bunge lijadili jambo halisi na dharura na muhimu kwa umma. Kifungu cha pili kinasema “Hoja ya namna hiyo itakuwa ni maalum na inaweza kutolewa wakati wowote hata kama majadiliano yatakuwa yanaendelea. Lakini baada ya kipindi cha maswali”.

Tatu, hoja itatolewa na Mbunge kwa kusimama mahali pake na kuomba idhini ya Spika kutoa hoja ya kuahirisha shughuli za Bunge kwa madhumuni ya kujadili jambo halisi la dharura na muhimu kwa umma. Nne kinasema, "Iwapo Spika ataridhika kwamba jambo hilo ni la dharura halisi na lina maslahi kwa umma, basi ataruhusu hoja hiyo itolewe kwa muda usiozidi dakika tano, na mjadala juu ya hoja hiyo utaendelea kwa muda amba Spika ataona unafaa kwa kuzingatia mazingira ya suala linalojadiliwa". Kwa hiyo, nasema iwapo Spika, ataridhika kwamba jambo hilo ni la dharura halisi na lina maslahi kwa umma.

Sasa kwa maana ya kwamba jambo hili, jana ndiyo tumepewa kwa mara ya kwanza taarifa kwamba kuna matatizo haya, na nyie wenyewe mlisshuhudia hata kwenye vyombo vya habari lonyeshwa. Jana tulahirisha kusudi wanaohusika wote wasimame waangalie linaendeleaje huko. Sasa leo hii sisi wenyewe tunamaliza baada ya kipindi hiki cha maswali, Waziri Mkuu atafunga Bunge. Kamati ya Ulinzi na Usalama inaondoka hapa inakwenda Dar es Salaam baada ya kikao hiki. Sasa cha dharura hapa kwamba ni dharura, kwa maana ya dharura, si kweli. Ni jambo lililotokea, tunalo. Kwa hiyo, mimi sijaridhika kwamba inafikiti vizuri katika Kanuni hii. Kwa hiyo, tunaendelea na Bunge. (*Makofi*)

Juu hapo Waheshimiwa Wabunge, tumekubaliana kwamba Ofisini kwetu Kamati ya Uongozi sikuishauri, tuchangie posho ya jana Wabunge wote na Wafanyakazi wote kwa ajili ya hawa wenzetu waliopata majeruhi. Tunaendelea na maswali. Nilisema Mheshimiwa Lucy Fidelis Owenya, atauliza swali la kwanza. (*Makofi*)

Na. 81

### **Idadi ya Maswali yanayojibiwa ndani ya Bunge**

**MHE. LUCY F. OWENYA** aliuliza:-

Je, kwa kipindi cha uhai wa Bunge Serikali inahitaji kujibu maswali mangapi?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, (SERA, URATIBU NA BUNGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Lucy Fidelis Owenya, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ibara ya 65 kifungo kidogo cha pili (2), uhai wa Bunge letu ni kipindi cha miaka mitano (5) chenye jumla ya Mikutano ishirini (20) yaani mikutano minne kila mwaka yenye vikao kadhaa kulingana na ratiba na matukio ya mkutano husika.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa kanuni za Kudumu za Bunge za mwaka 2007, zipo aina mbili za maswali ya Bunge. Aina ya kwanza ni maswali ya Mheshimiwa Waziri Mkuu yaliyofafanuliwa katika kifungo cha 38 (1) – (7) na aina ya pili ni maswali ya kawaida yaliyofafanuliwa katika kifungo cha 39(1) – (15).

Kwa mujibu wa kanuni hizo Maswali 15 yanapaswa kuulizwa kila siku katika mikutano ya kawaida na maswali 10 wakati wa mikutano ya bajeti, isipokuwa kwa siku za Alhamisi ambapo huanza na maswali kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu. Katika siku hizo, maswali 10 hujibiwa katika mikutano ya kawaida na maswali matano (5) hujibiwa katika mikutano ya Bajeti.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha uhai wa Bunge lililopita (2005-2010) jumla ya maswali 307 yaliulizwa na kujibiwa na Mheshimiwa Waziri Mkuu na jumla ya maswali ya kawaida 4,744 yaliulizwa na kujibiwa. Kama nilivyoeleza awali, idadi ya maswali hutegemewa na idadi ya siku kwa kila mkutano. Mathalani, kutokana na maandalizi ya uchaguzi mkuu wa Oktoba, 2010 idadi ya siku za mkutano wa Bajeti uliopita zilipunguzwa sana tofauti na mikutano mingine ya Bajeti.

Kwa mantiki hiyo, idadi ya maswali yanayoulizwa na kujibiwa katika kipindi kimoja cha uhai wa Bunge hutofautiana na kipindi kingine.

**MHE. LUCY F. OWENYA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kuniruhusu kuuliza swali ndogo la nyongeza. Namshukuru Mheshimiwa Waziri kwa majibu yake mazuri.

Kwa kuwa uhai wa kipindi cha Bunge siyo rahisi maswali yote kuweza kujibiwa. Je, Serikali haioni sasa ni muhimu kuwapatia Wabunge majibu kwa maandishi ili wakirudi katika majimbo yao waweze kuwaelezea wananchi kwamba walieleza matatizo yao na yakajibiwa kwa maandishi waweze kufanya kampeni zao kwa urahisi?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, URATIBU NA BUNGE):** Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema, kwanza niseme maswali yote yaliyoulizwa ni hayo 5,235. Kuthibitisha ukweli wa Mheshimiwa Lucy kwamba kuna maswali yalibaki. Kwa sababu yaliyojibiwa kati ya hayo ni 4,744 sawa na asilimia 90.62. Kwa hiyo, maswali yaliyobaki bila kujibiwa ni 491.

Mheshimiwa Spika, wanaopanga utaratibu wa kuuliza maswali ni Kamati ya Kanuni ya Bunge lako. Kwa hiyo, mimi nimelichukua wazo hili la Mheshimiwa Lucy nitalifikisha kwenye Kamati ya Kanuni ndiyo itakayoamua. Serikali itakuwa tayari kutekeleza lolote litakaloamuliwa na Bunge lako Tukufu. (*Makofi*)

**MHE. CONCHESTA L. MWAMIAZA:** Ahsante Mheshimiwa Spika, napenda kumwuliza Mheshimiwa Waziri kwamba kama mbunge akiuliza swali na asijibiwe na Waziri ambaye alipaswa kujibu hilo swali kama mimi nilivyofanyiwa na Mheshimiwa Kagasheki, Mbunge wa Manispaa. Naomba nipewe majibu nifanyeje?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, URATIBU NA BUNGE):** Mheshimiwa Spika, utaratibu ni kwamba swali linaulizwa kwa Serikali, sasa Serikali ni umoja wa *Front Bench* kuanzia Mheshimiwa Waziri Mkuu na Mawaziri wote ndiyo Serikali. (*Makofi*)

Ikitokea Waziri mmojawapo kati ya Mawaziri waliopo anaamini kwamba anayo majibu ya nyongeza anaweza kuisaidia Serikali. Sisi kwa utaratibu wetu anaruhusiwa kufanya hivyo. (*Makofi*)

Kwa hiyo, Mheshimiwa Kagasheki aliamini kwamba analo jibu la kumsaidia mwenzake aliyejibu swali la nyongeza.

Lakini si kila jibu, si wewe tu Mheshimiwa, inawezekana wako Wabunge wengi, na wengine wameniandikia hawatoshelezwi na majibu yanayojibiwa na Serikali kwa sababu yeye binafsi angetaka ajibiwe aina fulani.

Sasa kanuni ziko wazi, kama unaona hukuridhika na jibu ambalo Waziri amejibu, unaweza kumwomba Spika ukatoa hoja hapa na kulalamika hivyo ulivyolalamika na bado Spika anaweza kutaka Serikali ijibu. Vinginevyo unaweza ukarudisha tena swali hilo likajibiwa mara ya pili. Kwa hiyo, fursa hizo unazo. (*Makofi*)

Na. 82

### **Ujenzi wa hospitali ya Wilaya – Himo**

**MHE. AUGUSTINO L. MREMA** aliuliza:-

Serikali katika mwaka wa fedha 2010/2011 imeamua kujenga hospitali ya Wilaya kwenye mji mdogo wa Himo:-

- (a) Je, ni lini hospitali hiyo itaanza kutoa huduma kwa wagonjwa wa nje?
  
- (b) Je, ni lini wodi za kulaza wagonjwa zitakamilika ili wagonjwa wanaopaswa kulazwa hapo kwa matibabu waweze kupata huduma hiyo?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Augustino Lyatonga Mrema, Mbunge wa Vunjo, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, hospitali ya Wilaya ya Moshi ambayo imetokana na kupandishwa hadhi kwa kituo cha Afya cha Mji Mdogo wa Himo inatarajiwa kuanza kutoa huduma kwa wagonjwa wa nje mwezi Mei, 2011 mara baada ya kukamilika kwa mchakato wa manunuzi ya vifaa-tiba na samani na pia utaratibu wa usajili ili kupata mgawo wa dawa kutoka Serikalini.

Kwa sasa samani za thamni ya shilingi 10,840,000/= zimekwishanunuliwa na kufikishwa kituoni na vifaa vya thamani ya shilingi 26,000,000/= viro kwenye mchakato wa manunuzi na hadi mwisho wa mwezi Februari, 2011 vifaa vitakuwa vimekwishafungwa. (*Makofi*)

(b) Mheshimiwa Spika, ujenzi huu ulianza mwaka 2009/2010 kwa awamu ya kwanza ambapo jengo la wagonjwa wa nje lilikamilika, awamu ya pili ambayo ni mwaka 2010/2011 imepangiwa shilingi 300,000,000/= kwa ajili ya kuendeleza ujenzi.

Kutokana na usalama, Halmashauri imepanga kuanza na ujenzi wa uzio, choo cha nje, jengo la utawala na jengo la huduma za mionzi. Kwa sasa mkandarasi amekwishaanza kazi. Awamu ya tatu ni kujenga wodi ya wagonjwa. Maombi ya fedha ya ujenzi huo yataingizwa katika mpango wa 2011/2012. (*Makofi*)

**MHE. AUGUSTINO L. MREMA:** Kwanza naomba niipongeze Serikali kwa jinsi inavyohudumia mji wa Himo. Naomba nipongeze kwa sababu ni juzi tu Rais ametoa shilingi milioni 150 kwa ajili ya usambazaji wa maji na sasa hivi wanalipwa milioni 300 kwa ajili ya ujenzi wa hiyo hospitali. (*Makofi*)

Swali la nyongeza. Kulingana na malengo ya *millennium development goals* ni kwamba Serikali zote duniani zinatakiwa ziwekeze watoto wachanga walio chini ya miaka mitano wanatibiwa bure, wa mama wajawazito wanapata matibabu ya bure na wazee.

Serikali inaweza kunihakikisha kwamba hospitali hii itakapoanza watahakikisha watoto wadogo wa Vunjo wanatibiwa bure bila gharama zozote wa mama wajawazito badala ya kwenda hospitali na kudaiwa pamba, *gloves*, nyuzi na mambo kama hayo na wenyewe wakapatiwa matibabu ya bure na wazee walioko Vunjo na wenyewe watatiwa bure kulingana na *millennium development goals* za Umoja wa Mataifa?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Spika, naomba nichukue nafasi

hii kukushukuru Mheshimiwa Lyatonga Mrema, kwa pongozi hizo na unavyoonyesha jinsi ambavyo Serikali hii ni makini katika kutekeleza majukumu yake.

Pili, haya aliyoyleza hapa yote, wala sidhani kama ni swali kwa sababu najua Mheshimiwa Mrema amekuwa Serikalini anafahamu kabisa. Watoto wote wenye umri wa miaka mitano kwenda chini kwa mujibu wa Sera za Serikali yetu na utaratibu wetu wanatibiwa bure kwa maana ya kwamba wazazi wa watoto hao hawatozwi kutoka mfukoni, kwa sababu hakuna bure kwa maana ya bure kama inavyowekwa.

Lakini bure kwa maana ya kutokumtoza mzazi kutoka mfukoni mwake. Pili, kwa upande wa akina mama ambao wanakwenda pale wakina mama wale wote wanapokwenda kwa ajili ya *gloves* na nyembe na vitu vingine wale hawapashwi kulipa chochote pale. Na hili la wazee nalo hivyo hivyo limekuwa limewekwa hivyo.

Kwa hiyo, hawa wananchi wanaotoka katika Jimbo la Vunjo ni Watanzania, na wao wana-*enjoy* utaratibu huu. Sasa inawezekana humu ndani kuna watu wengine ambao wakienda pale na tukijua kwamba kuna mtu amefanya kinyume na hivyo, basi sisi tutachukua hatua. Lakini nataka nithibitishe kwamba wananchi hawa watapata huduma hizo kwa utaratibu huo nilioueleza.

**MHE. JOSEPHINE J. NGENZABUKE:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa, Hospitali ya Mkoa wa Kigoma inahudumia wilaya mbili, wilaya ya Kigoma Vijijini na Kigoma Mjini. Je, ni lini Serikali itajenga hospitali ya Wilaya ya Kigoma Vijijini?

**SPIKA:** Lakini haya ni maswali mengine kabisa jamani, sio ya nyongeza. Haya Mheshimiwa Naibu Waziri, jibu. Maana unayajua hayo mambo.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba nijibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Ngenzabuke, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa bahati nzuri sana ninapozungumza hapa nimetoka Kigoma na Tabora. Hili tatizo ambalo Mheshimiwa Mbunge, analizungumzia hapa ni kweli kwamba liko pale.

Mheshimiwa Spika, kinachofanyika sasa hivi ni kwamba pale kwenye Manispaa ya Kigoma, kwa sababu Manispaa ya Kigoma wapo karibu sana na hii wilaya, pale pameanzishwa *Baptist Hospital* ambayo ni *Designated Hospital*, Hospitali Teule, ambayo itakuwa inawasaidia wananchi waliopo jirani pale, lakini bado itakuwa hajitatua tatizo hili. Kwa hiyo, wanaangalia maeneo ya Kaziramimba na maeneo mengine kuona kwamba hospitali hii iweze kujengwa. Sasa utaratibu wa Serikali ni kwamba, tunapokuwa tumeanzisha wilaya pale tunatakiwa tuwe na hospitali ya wilaya.

Kwa hiyo, jambo hili ni jambo ambalo Mheshimiwa Mbunge na wenzake wanatakiwa washirikiane kuhakikisha kwamba wanalileta sasa kwa utaratibu ule ambao tunaujua kwa sababu lina *budget implications* zake ili tuweze kuliingiza katika mpango. Lakini ni jambo muhimu analolizungumza na mimi ninamwunga mkono kwamba kuna haja ya kulisukuma jambo hili.

**MHE. TUNDU A. M. LISSU:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa, Serikali imekuwa inasema kwamba matibabu kwa wazee na kwa watoto ni Bure. Lakini katika hali halisi wazee wanakwenda hospitali wanaambiwa kama huna 5,000/= hakuna tiba, watoto wanapelekwa hospitali huna 5,000/= hakuna tiba. Je, Serikali imechukua hatua gani dhidi ya hizo mamlaka za hospitali ambazo zinaendelea kutoza wazee, akina mama na watoto fedha ili watibiwe?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Tundu Lissu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, hapa ninazungumzia sera Mheshimiwa Mbunge na kama kuna kitu cha namna hiyo kinafanyika, naomba utupatie majina ya hao wanaofanya hivyo kwa sababu, hizi ni sera za Serikali hapa. Mimi hapa ninasema wala sibabaishi, ni jambo ambalo ninalifahamu. Kama zipo *particular hospitals* ambazo unazijua zinakwenda kinyume na maelekezo haya ninayoyatoa hapa, tunaomba tupatiwe majina ya hao wanaohusika ili tubanane nao. (*Makofi*)

Ninataka nichukue nafasi hii kuwaonya wale wote ambao wanafanya hivyo, ni kinyume kabisa cha maelekezo ya Serikali. Hawapaswi kufanya hivyo kabisa. Kwa hiyo, kama unayo majina na wengine wenyewe majina watuletee. (*Makofi*)

**SPIKA:** Nadhani nilimsikia Naibu Waziri wa Afya, kwamba Serikali imejiandaa utaratibu wa kutoa vitambulisho kwa wazee; maana wanatendewa hivyo. Mheshimiwa Kepteni John Chiligati, swali linalofuata.

Na. 83

### **Tatizo la maji-vijiji vya jimbo la Manyoni**

**MHE. KAPT. JOHN Z. CHILIGATI** aliuliza:-

Katika kutekeleza mradi wa maji wa Bonde la Ufa mwaka 1970, Kata ya Sasajila na Majiri ilijengwa miundombinu kadhaa kama vile, visima vinne vilichimbwa, matanki ya kuhifadhia maji yalijengwa kwenye vijiji vinne na mtandao wa mabomba. Lakini baadaye mradi huo ulikufa kutokana na kung'olewa kwa mabomba:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuufufua mradi huo, ili kuondoa tatizo kubwa la maji linalowakabili wananchi wa vijiji vilivyo jirani na mradi huo vya Mpandagani, Chinangali, Chibumagwa na Chinyika?

## **NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI) alijibu:-**

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Kapt. John Zefania Chiligati, Mbunge wa Manyoni Mashariki, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mradi wa Bonde la Ufa ulijengwa miaka ya 1970 ukihusisha vijiji vya Chibumagwa, Mpandagani, Chinangali, na Majiri. Chanzo cha Maji cha mradi huu wa pamoja (*Grouped Scheme*) kilikuwa ni visima virefu vinne (4) vilivyochimbwa katika Kitongoji cha Msachile, Kijiji cha Chibumagwa. Mradi huu ulitoa huduma kwa muda mfupi na ukasimama kutokana na kuhujumiwa kwa kukatwa mabomba ya mradi. Kwa sasa mradi huo unahudumia kijiji cha Chibumagwa peke yake, ingawa uendeshaji wake si wa kuaminika kwa sababu ya uchakavu. Katika kipindi hicho kwenye kijiji cha Sasajila kulijengwa mradi amba o na kwa sasa haufanyi kazi.

Mheshimiwa Spika, miradi hii miwili kimsingi imeshindwa kukidhi matarajio ya utekelezaji wake, kutokana na wananchi wa vijiji hivyo kushindwa kutekeleza majukumu yao ya kulinda miundombinu na kugharamia uendeshaji na matengenezo ya miradi. Aidha, kutokana na ukosefu wa ulinzi imara wa miradi hii, imehujumiwa na kuibiwa mashine, vipuri na mabomba.

Mheshimiwa Spika, kwa sasa Serikali inatekeleza Programu ya Kuendeleza Sekta ya Maji (*WSDP*). Kupitia programu hiyo, Halmashauri zote za Wilaya nchini zinatekeleza programu ndogo ya Maji Vijijini na Usafi wa Mazingira (*RWSSP*). Utekeelzaji wa programu hiyo unahuishwa vijiji 10 kila Wilaya kwa kila awamu.

Mheshimiwa Spika, katika utekelezaji wa Programu ya maji vijijini, kijiji cha majiri ambachoni mionganoni mwa vijiji vilivyojua katika mradi wa pamoja (*Grouped Scheme*) kiko katika awamu ya kwanza inayoendelea kutekelezwa ambapo usanifu wa mradi umekamilika.

Vijiji vingine katika kundi la awali havikuweza kuunganishwa kwenye mradi wa maji wa majini kwa sababu maji yaliyopatikana kwenye kisima cha majili yaliweza kutosheleza mahitaji ya kiji cha Majiri tu.

Mheshimiwa Spika, uwezo wa kujitegemea kwa Halmashauri ya Wilaya ya Manyoni ni asilimia tatu (3) tu, hivyo ni dhahiri kuwa utekelezaji wa miradi katika vijiji hivi hauwezi kutekelezwa kupitia fedha za ndani (*own source*). Halmashauri inaendelea kuhamasisha vijiji vya Mpandagani, Chinangali, Chibumagwa, Chinyika na Sasajila ili viweze kuunda vyombo vya watumiaji maji na kuanzisha mifuko ya maji ili viweze kutekeleza miradi ya maji kwenye awamu zitakazofuata chini ya Programu ya Maji.

Aidha vyanzo vingine vya rasilimali fedha vitafikiriwa ikiwa ni pamoja na fedha zitakazotokana na ruzuku ya maendeleo ya Serikali za Mitaa (*LGDG*).

**MHE. KAPT. JOHN Z. CHILIGATI:** Mheshimiwa Spika, namshukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa majibu mazuri, sahihisho dogo tu ni kwamba katika mradi ule mashine wala vipuri vya visima vile havikuibiwa, viro na visima viro. Maswali mawili madogo ya nyongeza:-

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa, taarifa ya Mheshimiwa Naibu Waziri, inasema kwamba maji kupitia mradi wa *World Bank* pale Majiri, yanatosha kwa kijiji kimoja tu. Vile vijiji vingine vya Chinangali, Mpandagani na Chibumagwa, hayatoshelezi. Sasa swalii ni kwamba, kwa vile visima viro na matenki yapo. Je, Wizara ya *TAMISEMI* haiwezi kushirikiana na Wizara ya Maji ili mradi huu ufufuliwe kwa vile kuna vijiji ambavyo havijaguswa na mradi huu wa *WORLD BANK*?

Mheshimiwa Spika, swalii la pili. Kwa kuwa uchimbaji maji katika kijiji cha Kintinku, katika mradi huu wa *World Bank*, maji yamekosekana. Na kwa kuwa, katika muinuko wa Mbwasa, kuna visima vinne vilivyo chimbwa na *KONOIKE* wakati wanajenga barabara ya lami ya Dodoma – Manyoni na maji akavuta yeye mpaka Kintinku, na mradi ulipokwisha vile visima amevikabidhi kwa Serikali.

Je, Serikali sasa inaweza kumwambia Mkandarasi wa *World Bank*, kwamba kwa sababu Kintinku maji yamekosekana, visima vile ambavyo viro pale Mbwasa, sasa vitumike kupeleka maji Kintinku?

Kwa kufanya hivyo vijiji vya njiani kama Maweni, Mvumi, Ngaicho, Msilile, navyo viingizwe katika mradi huo?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza na pia ninapokea haya masahihisho ambayo Mheshimiwa Mbunge, ameyatoa hapa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa kuhusu hili la kile kijiji cha Majiri anachokizungumzia. Labda ili Bunge lako Tukufu liweze kupata picha kamili, mradi ule ili kuukamilisha pale unahitaji milioni 667. Sasa hapa vinazungumzwa vijiji vinne zidisha mara nne, unazungumza habari ya bilioni 2.8.

Mheshimiwa Spika, nataka nimwambie tu Mheshimiwa Chiligati, kwamba natambua amekuwa Serikalini kwa muda mrefu. Jambo analolizungumza hapa ni jambo kubwa na hawa wananchi wanapata matatizo huko waliko. Nataka nimwambie kwamba sisi kama Serikali, tatizo hilo tunaliona na tutashirikiana naye tuone kwamba tunafanya nini ili kuwaondoa hawa wananchi katika hali hii ambayo yeye anaizungumzia hapa.

Mheshimiwa Spika, la pili amezungumzia kuhusu hiki chanzo ambacho kinatokea Kintinku, nacho hivyo hivyo kina gharama zake. Mimi ninachofikiri hapa ambacho kinaweza kufanyika ni kumpata Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri hii pamoja na wale wengine, na Profesa Mwandosya ananisikiliza hapa yupo humu ndani ya Bunge na kama anaweza kunisaidia atanisaidia.

Haya ni mabilioni ya hela, nikisema tu hapa haraka haraka kwamba ndio tutaoa hizo hela na huyu dada aliyekaa hapa ataniuliza wewe umesema zile bilioni utatoa utazitoa wapi sasa, kwa maana ni suala la Bajeti. Lakini mimi na wenzangu tupo tayari tukashirikiana na Mheshimiwa Chiligati, ili tuweze kuona kwamba tunaondoka katika tatizo hili.

Na. 84

### **Kupeleka Maji ya Ziwa Victoria Nyamagana**

**MHE. EZEKIA D. WENJE** aliuliza:-

Jimbo la Nyamagana licha ya kuwa karibu sana na Ziwa Victoria lina tatizo kubwa la maji safi na salama, na maji ya ziwa hilo yanaweza kusafirishwa kwenda maeneo mengine ya Shinyanga na kuyaacha maeneo kama Isebanda, Sawa, Kanindo na Fumagira, kwenye Jimbo la Nyamagana yakiwa hayana maji:-

- (a) Je, kwa nini Serikali isione kuwa ni busara kufikisha maji ya Ziwa Victoria kwenye maeneo yaliyo jirani na Ziwa hilo kabla ya kufikiria kuyapeleka kwenye maeneo ya mbali?
- (b) Je, Serikali ina mpango gani sasa wa kupeleka maji safi na salama kwenye maeneo yaliyoainishwa kwenye swali hili?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Maji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ezekia Dibogo Wenje, Mbunge wa Jimbo la Nyamagana, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inatekeleza programu ya maji vijiji ambapo Halmashauri ya Jiji la Mwanza, ilishachagua vijiji 10 vya kipaumbele, ambavyo ni Nyafula, Sangabuye, Kabusungu, Kayenze, Igogwe, Nyamulolelwa, Kahama, Nyamadoke, Lwanhima na Fumagira, ambavyo vitatekeleza programu hiyo. Maeneo ya Isebanda na Sawa, ni vitongoji vya kiji cha Lwanhima na Kanindo, ni kitongoji cha kijiji cha Fumagira.

Mheshimiwa Spika, kulingana na Sera ya Taifa ya Maji, Vijiji vina jukumu la kuchagua teknolojia wanayoitaka. Katika Jiji la Mwanza, jukumu hilo linatekelezwa kwa ushauri wa Halmashauri na Mtaalam Mshauri, aliyeajiriwa na Halmashauri. Vijiji vya

Lyamhina na Fumagira, vilichagua teknolojia ya visima virefu kama chanzo chao cha maji badala ya chanzo cha maji ya ziwa Viktoria. (*Maklofi*)

Mheshimiwa Spika, hadi sasa hatua ya utekelezaji iliyofikiwa hadi sasa ni kuwa, tarehe 22/7/2009 Halmashauri iliajiri Mtaalam Mshauri, ambaye ni *KOWI – Tanzania Consulting Engineers & Planners Ltd. in association with ENV Consult Tanzania Ltd.*

Vilevile tarehe 4/2/2011 Halmashauri ilimwajiri Mkandarasi wa kuchimba visima virefu, ambaye ni *Mass Drilling Company Ltd*; ataanza kuchimba visima vya maji tarehe 28/2/2011. Atakapomaliza kuchimba visima na maji kupatikana, Mtaalam Mshauri atafanya usanifu wa kina wa miradi kwa ajili ya vijiji vyote 10 vilivyochedguliwa na kuanda makabrasha ya zabuni ili kupata Mkandarasi atakayejenga miundombinu ya maji katika vijiji husika.

Mheshimiwa Spika, uchimbaji wa visima utaanza katika vijiji vya Nyafula, Kahama, Nyamadoke, Nyamulolelwa na Igogwe, ambapo baadaye uchimbaji utafanyika katika vijiji vya Kabusungu, Kayenze, Lwanhima, Fumagira na Sangabuye. Utekelezaji wa mpango nilioueleza utakapokamilika, maeneo ya Isebenda na Sawa, katika kijiji cha Lwanhima na Kanindo katika kijiji cha Fumagira, yaliyoainishwa na Mheshimiwa Mbunge, yatapata huduma ya maji.

**MHE. EZEKIA D. WENJE:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri kutoka kwa Naibu Waziri, napenda niulize maswali mawili madogo ya nyongeza. Kwanza katika hivyo vijiji 10 alivyovitaja, ni vijiji viwili tu ndio vinapatikana katika Jimbo la Nyamagana, vijiji 8 viro katika Jimbo la Ilemela. Lakini pia katika kijiji cha Luanhima na Fumagira, hivi vijiji vina *geographical coverage* kubwa sana, lakini pia sasa haja-*indicate* kwenye majibu yake kwamba hivi visima vitakavyochimbwa kila kijiji kitachimbiwa visima vingapi, haja-*indicate* kwenye majibu.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, swali la kwanza ni kwamba ninaomba nielewe kwamba visima hivi, kwa mfano kijiji cha Luanhima, ni visima vingapi vitachimbwa hapo?

Kwenye kijiji cha Fumagira, ni visima vingapi vitachimbwa? Kwa sababu ukiangalia *geographical coverage* na ukitoka Luanhima kwenda Isebanda, ni *almost* kilometra 2 mbalimbali.

Kwa hiyo, tukichimba kisima 1 tu kule Isebanda, haitasadia watu wangu; mimi nimetumwa kuja kudai maji ya Ziwa Viktoria. Sasa naomba Waziri anieleze kwamba Serikali inaona tabu gani kupeleka maji ya Ziwa Viktoria kwenye hivyo vijiji ili angalau vinavyopita njiani, wakazi wa hayo maeneo wanaweza wakavuta wakapeleka majumbani mwao.

Mheshimiwa Spika, nashukuru.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Maji, naomba kujibu maswali ya nyongeza ya Mheshimiwa Wenje, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa nikiri kwamba sitaweza kukuambia idadi ya visima. Ila ni kwamba katika utafiti au usanifu ambaou umefanyika, yule mtaalam ndio ataainisha ni visima vingapi vitatosheleza mahittaji husika katika kila kijiji. Kwa hiyo, mtaalam ambaye yupo anafanya utafiti ataainisha ni visima vingapi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kutoa maji kwenye ziwa ni kwamba hakuna anayekataa kutoa maji kwenye ziwa ila ni kwamba ukitoa maji kwenye ziwa ni gharama zaidi kuliko ukitumia visima virefu. Na maji ya ziwa yanahitaji kuweka dawa nyingi ili yawe maji safi na salama kwa matumizi yetu. Lakini yale ya visima virefu kidogo huwa ni safi na yanahitaji madawa kidogo kidogo sana ili yaweze kutumika bila madhara kwa binadamu. Kwa hiyo, vijiji vinaamua ni teknolojia ipi watumie. Lakini ikibidi kwamba hakuna visima, tutachukua maji kutoka kwenye ziwa Viktoria. (*Makofi*)

**MHE. DKT. MAUA ABEID DAFTARI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Spika, lakini nina swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa juhudini nzuri za kusambaza maji ya Ziwa Viktoria, zimefanyika na zimesaidia sana wananchi wa Shinyanga na Vitongoji vyake. Na kwa kuwa, sasa juhudini zinaendelea kusambaza maji hayo katika maeneo mengine.

Je, Mheshimiwa Waziri, atatuhakikishiaje usalama wa vyombo vyaa usafiri wa ziwa hili, wakati maji yanaendelea kupungua?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Maua Daftari, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nikiri kwamba maji ya ziwa Viktoria yatapungua jinsi tunavyotumia. Lakini ili tuweze kufanya maji ya ziwa yasipungue, tutahitaji kuhifadhi vyanzo vyaa maji ili maji mengi yaendelee kuingia ndani ya ziwa Viktoria. Kwa hiyo, ni lazima kutakuwa na *balance*. (*Makofi*)

Na. 85

#### **Tatizo La Maji Safi na Salama - Ukonga**

**MHE. NEEMA MGAYA HAMID (K.n.y. MHE. EUGEN E. MWAIPOSA)** aliuliza:-

Kwa muda mrefu sana maeneo yote ya Jimbo la Ukonga yanakabiliwa na tatizo kubwa la upatikanaji wa maji safi na salama toka *DAWASCO*. Tatizo hili limekuwa suga na limesabisha maisha ya wakazi wengi wa Ukonga, hasa wanawake kuwa magumu sana:-

- (a) Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha kwamba tatizo hili linapatiwa ufumbuzi wa kudumu?
- (b) Kwa kuwa, tatizo la maji limekuwa sugu katika Jiji la Dar-es-Salaam. Je, Serikali haioni umuhimu wa kuanza Operesheni Maji Kwanza, kama ilivyofanya kwenye Kilimo Kwanza?
- (c) Je, ni kwa kiwango gani mradi wa kuboresha huduma ya maji safi na taka uliogharimiwa dola milioni 164.4 na Benki ya Dunia, Benki ya Maendeleo ya Afrika, Benki ya Rasilimali ya Jumuiya ya Ulaya, DAWSCO na DAWASA mwaka 2003 – 2007 uliweza kutatua tatizo la uhaba wa maji hususan katika jiji la Dar-es-Salaam?

**SPIKA:** Haya, Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

Unasubiri kuitwa eeh! Kama unataka kusimama unasimama halafu unasubiri unaitwa kwa jina.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Maji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Eugen Mwaiposa, Mbunge wa Ukonga, lenye vipengele (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, ili kuhakikisha kuwa tatizo la uhaba wa maji katika Jimbo la Ukonga linapatiwa ufumbuzi wa kudumu, Serikali ina mpango wa kuchimba visima virefu 20 vya maji chini ya ardhi katika maeneo ya kimbiji na mpera. Visima hivyo vitatoa huduma ya maji kwenye kata za Kitunda, Ukonga, Yombo Vituka, Kipawa, Kiwalani, Kinyerezi, Segerea na Tabata katika Jimbo hilo la Ukonga.

(b) Mheshimiwa Spika, Serikali kwa kuzingatia umuhimu wa maji kwa ustawi wa kiuchumi na kijamii imepanga kuongeza Bajeti kuanzia Mwaka wa Fedha 2011/2012 kwenye sekta ya maji. Pia inatekeleza programu ya maendeleo ya sekta ya maji nchini, ikiwa ni pamoja na Jiji la Dar-es-Salaam.

Tayari Serikali, imeandaa mpango maalum kwa ajili ya kuboresha huduma ya maji katika Jiji la Dar-es-Salaam. Utekelezaji wa mpango huo ambao utazalisha maji yanayokidhi mahitaji, utaanza mwezi Agosti, 2011 na kukamilika mwezi Desema, 2013. (*Makofi*)

(c) Mheshimiwa Spika, mradi wa kuboresha huduma ya maji safi na maji taka uliogharimiwa na Benki ya Dunia, Benki ya Maendeleo ya Afrika na Benki ya Rasilimali ya Ulaya kwa kiasi cha dola za kimarekani milioni 164.4 pamoja na kazi nyingine, zilijumuisha ukarabati wa mitambo ya maji safi Mtoni, Ruvu Chini na Ruvu Juu.

Utekelezaji wa mradi huo umeongeza uwezo wa uzalishaji wa maji safi na salama kutoka wastani wa lita za ujazo milioni 225 kwa siku hadi lita milioni 300 kwa siku.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu ya Mheshimiwa Waziri, nina swali moja la nyongeza. Katika majibu yake ya msingi Mheshimiwa Naibu Waziri amezungumzia visima vya Kipiji ambavyo amevitaja viko Ukonga, lakini ninavyofahamu ni mradi wa Kigamboni, mradi huu mpana wa Kibiji. Lakini swali langu linahusu uwekezaji huu wa miradi ya maji ya Benki ya Dunia na wadau wengine kama alivyozungumza. Mitandao hii inahusu Ruvu Juu na Ruvu Chini ambayo pamoja na Ukonga inagusa vilevile Jimbo la Ubungo.

Hali ilivyo hivi sasa ni kwamba, pamoja na kuwekwa kwa mtandao wa maji maarufu kama mabomba ya Wachina, maji katika Kata mbalimbali za Kwembe, Msigani, Mbezi, Kimara, Saranga hayatoki. Je, Naibu Waziri yuko tayari kwenda kutembelea eneo la miundombinu ili kuondokana na kasoro mbalimbali ikiwemo tatizo la upotevu wa maji la uunganishaji kiholela la wafanyabiashara wanaouza maji kwa bei mbaya na hivyo kusababisha pamoja na uwekezaji pesa, maji hayatoki hata baada ya miundombinu kuboreshwa?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, kwanza nampongeza Mheshimiwa Mnyika kwa kuwa amelipa suala la maji kipaumbele katika shughuli zake za kila siku na suala la kutembelea nitapanga na nitamwalika Mheshimiwa Mnyika twende wote tukakague kazi ambazo zinaendelea katika jiji la Dar es Salaam.

**MHE. DAVID E. SILINDE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi niulize swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa kero ya maji kama inavyoonekana katika Jimbo la Ukonga limekuwa likielezewa karibu katika maeneo mengi ya Tanzania ikiwemo Mbozi Magharibi: Je, ni kwanini sasa Serikali isitupe tathimini na ni lini itakuwa na uhakika wa kutatua tatizo la maji katika Jamhuri ya Muungano Tanzania ili kero hii iondolewe kabisa? (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante. Afadhali hukusema Dar es Salaam inafanana na Mbozi. (*Kicheko*)

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba tunaelewa kwamba huduma ya maji ni tatizo karibu nchi nzima na ndiyo maana ndani ya ilani ya Chama cha Mapinduzi tumeagiza kwamba tutaongeza bajeti ya Serikali ili tuweze kutatua matatizo hayo ikiwa ni pamoja na Mbozi. Kwa hiyo, baada ya hapo tutakuwa na wastani wa asilimia karibu 60 ya maji vijijini. Watapata huduma ya maji baada ya miaka mitano ndani ya ilani ya Chama cha Mapinduzi.

## **Fedha kwa Ajili ya Kukarabati Miundombinu ya Maji**

**MHE. JEROME D. BWANAUSI** aliuliza:-

Wakati wa Kampeni za Uchaguzi Mkuu Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete aliahidi kutoa fedha kwa ajili ya ukarabati wa miundombinu ya usambazaji maji iliyochakaa ambayo iliwekwa tangu mwaka 1955 kutoka chanzo cha Chiwambo kilichopo Lulindi ambacho kinahudumia Kata za Lulindi, Namalenga, Mchauru, Mbuyuni na Chiungutwa na tatizo la ukosefu wa maji limekuwa kubwa sana kwa hivi sasa:-

Je, ni lini Serikali itaanza kutekeleza ahadi hiyo ya Mheshimiwa Rais ili kuwashukuru wananchi wa Lulindi na tatizo hilo?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Maji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Jerome Dismas Bwanausi, Mbunge wa Lulindi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mradi wa maji wa Chiwambo uliopo katika Jimbo la Lulindi Wilayani Masasi ni wa maji ya mitiririko ambao ulibuniwa kuhudumiwa vijijini vilivyoko katika Kata tano za Lulindi, Namalenga, Mchauru, Mbuyuni na Chiungutwa.

Mradi huo ambao unatoa maji kutoka chemchemi za Chiwambo ulijengwa miaka mingi iliyopita mwaka 1955, hivyo miundombinu yake imechakaa. Mwaka 2009 timu ya wataalam kutoka Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Mtwara, Halmashauri ya Wilaya ya Masasi na Wizara ya Maji ilikagua mradi na kufanya tathmini kwa lengo la kubaini mahitaji ya fedha kwa ajili ya ukarabati wa mradi. Tathmini hiyo ilionesha kuwa ukarabati utahitaji shilingi milioni 580.

Mheshimiwa Spika, Serikali tayari imeanza kutekeleza ahadi ya Mheshimiwa Rais kwa kutenga shilingi milioni 50 katika bajeti ya mwaka wa 2010/2011. Fedha hizo ambazo zilitumwa Halmashauri ya Wilaya ya Masasi zitatumika katika kununua na kufunga mabomba makubwa zaidi yenye kipenyo wa inchi nane na urefu wa kilomita 11 kutoka kwenye chanzo cha maji kwenye chemchemi hadi kwenye matanki ya kuhifadhi maji. Hii itawezesha maji mengi zaidi kuingia kwenye matanki kwa ajili ya matumizi. Ahadi ya Mheshimiwa Rais itatekelezwa kwa kutenga fedha zaidi katika bajeti ya mwaka 2011/2012 kwa ajili ya kukarabati mradi wa Chiwambo.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa huu ni mradi wa Halmashauri ya Wilaya ya Masasi, Halmashauri inabidi iupe kipaumbele kuuweka katika mipango yake pamoja na kuutengea fedha. Mchango wa Serikali katika mradi huu na mingine ya aina hiyo ni kuunga mkono juhudzi za Halmashauri ili kuimarisha dhana ya Halmashauri kumiliki miradi hiyo.

**MHE. JEROME DISMAS BWANAUSI:** Mheshimiwa Spika, kwanza napenda kuchukua nafasi kumshukuru sana kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji. Lakini nina maswali mawili madogo ya nyongeza:-

La kwanza, kwa kuwa Mheshimiwa Rais, alipofika pale baada ya kupokea taarifa juu ya uwezo mdogo wa Halmashauri katika kutekeleza mradi huu ndipo alipoahidi kwamba utekezaji wa mradi huu utaanza katika kipindi cha mwaka 2010/2011 na kumalizwa katika kipindi cha mwaka 2011/2012. Je, katika kuthamini, kuenzi na kutii ahadi ya Mheshimiwa Rais: Je, Serikali itahakikisha kwamba mradi unawekwa katika bajeti ya mwaka 2011/2011 ili utekelezwe kwa pamoja?

La pili, je, Serikali imejipanga vipi katika kutekeleza mradi huu ambaou unahitaji fedha nyingi kama alivyoainisha, shilingi milioni 580? Je, watatumia wataalam ama watahakikisha kwamba tunapata mkandarasi mwenye sifa ili autekeleze mradi huu kwa uhakika? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba Rais alipotembelea kule alitoa ahadi na ahadi zote ambazo Rais ametoa, Serikali itaweka kipaumbele katika kuweka bajeti yake kwa sababu Mkuu wa Serikali ni Rais. Kwa hiyo, Rais akishasema, basi sisi tutaweka kipaumbele kwenye bajeti.

Mheshimiwa Spika, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba fedha hizo zinazohitajika tutatafuta kila namna ziweze kupatikana ili mradi ule uweze kukamilika na wananchi wa Masasi waweze kupata maji?

**MHE. JUMA A. NJWAYO:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi kwa kuwa matatizo yaliyoko katika mradi huu wa Chiwambo, unafanana kabisa na matatizo yaliyoko katika mradi mdogo wa Mahuta Mjini, kiasi cha kusababisha wananchi wa vijiji vya Mtoni, Nakayaka, Mahuta kwenyewe, Uwongo, Lubangala na Luhunga kupata matatizo makubwa sana ya maji. Je, Serikali sasa inaweza kuangalia mradi huu ukaenda sambamba na ule wa Chiwambo katika kutatua matatizo ya maji?

**WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, kwanza namshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri sana anayoendelea kuyatoa kwa niaba ya Wizara. (*Makofi*)

Pili, naomba nimtaarifu Mheshimiwa Njwayo kwamba miradi anayoisema na vijiji anavyovisema viko katika mradi mkubwa wa Makonde, ambaou tunaufanya tathmini mpya. Sasa tunaye mtaalam mwelekezi ambaye karibu anakamilisha kazi ili tuweze tukaufanya ukarabati mkubwa mradi huo. Naamini katika kutekeleza huo baada ya kupata ushauri wa mshauri mwelekezi tutazingatia vijiji hivi vyote alivyovitaja.

### **MHE. GODFREY WESTON ZAMBI aliuliza:-**

Ili kauli mbiu ya Kilimo Kwanza iweze kuwa na maana zaidi, kuna umuhimu wa kufanya pembejeo za kilimo na zana za kilimo kupatikana kwa wingi kwa bei nafuu zaidi:-

Je, Serikali imejiandaaje, kuhakikisha kwamba pembejeo za kilimo hususan mbolea na mbegu za kilimo vinapatikana kwa wingi, kwa wakati na kwa bei nafuu ili wakulima walio wengi wakiwemo wadogowadogo waweze kumudu?

### **NAIBU WAZIRI WA KILIMO CHAKULA NA USHIRIKA alijibu:-**

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Godfrey Weston Zambi, Mbunge wa Mbozi Mashariki, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Kilimo Kwanza ni Azma ya Taifa ya kuongeza kasi ya kuleta mapinduzi ya kijani katika sekta ya Kilimo. Katika kufanikisha azma hiyo, Serikali inatekeleza mpango wa ruzuku ya pembejeo za mazao nchini ili kuhakikisha kuwa pembejeo za kilimo hususan mbegu bora na mbolea zinapatikana kwa wingi, kwa wakati na kwa bei nafuu.

Katika msimu 2010/2011, kwa kutumia utaratibu wa vocha, Serikali imetoea ruzuku kwa tani 200,000 za mbolea na tani 20,000 za mbegu bora ambazo zimelenga kuwafikia wakulima 2,000,000 wanaolima mahindi na mpunga.

Aidha, Serikali imetoea ruzuku ya mbolea na madawa ya pamba yenye thamani ya shilingi bilioni nane katika msimu huu wa kilimo.

Mheshimiwa Spika, tunayo gesi asilia hapa nchini na tunaangalia uwezekano wa kuitumia. Ili kujenga uwezo wa kuzalisha mbolea kutokana na gesi asilia tuliyonayo, Serikali inashauriana na makampuni ya *Polyserve*, *Deepack*, *Helm* na *Tanzomin* ili kujenga kiwanda kikubwa cha mbolea nchini. Pamoja na hivyo, kiwanda cha mbolea cha Minjingu kinachozalisha mbolea ya *Phosphate* kitaimarishwa ili kufikisha huduma zake kwa wakulima.

Mheshimiwa Spika, tarehe 13 Januari, 2011, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania - Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete alizindua mradi wa kuingiza mbolea kwa wingi nchini unaotekelizwa na kampuni ya *YARA*. Lengo ni kuhakikisha upatikanaji wa mbolea unakuwa wa uhakika kwa muda wote. Kampuni hiyo, imekubali kuwekeza nchini na kwa kuanzia, imeanza kujenga ghala lenye uwezo wa kuhifadhi tani 40,000 kwa wakati mmoja huko Kurasini, Dar es Salaam. Mradi huo unatarajiwa kukamilika katika kipindi cha miaka miwili.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu, kupitia wakala wa mbegu za Kilimo (*Agricultural Seed Agency*) inashirikiana na Jeshi la Kujenga Taifa na Jeshi la Magereza kuongeza uzalishaji na usambazaji wa mbegu bora nchini.

Aidha, Serikali inakamilisha maandalizi ya mpango wa kujitosheleza kwa mbegu mama za kilimo kwa kushirikisha sekta binafsi, kuzalisha mbegu za msingi (*foundation seed*) kwa niaba ya wakala wa mbegu za kilimo, yaani ASA na kuzalisha kwa wingi mbegu bora za kutosha kwa matumizi ya nchi yetu *certified seed*. Katika mpango huu, mashamba ya mbegu ya Taifa yatakarabatiwa na kujengewa miundombinu ili yatumike kuzalisha mbegu mama. Aidha, uzalishaji wa mbegu bora kwa wakulima utafanywa na sekta binafsi chini ya usimamizi wa Wakala wa Mbegu.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu inampongeza sana Mheshimiwa Godfrey Zambi kwa swali zuri na uhamasishaji wa kilimo bora katika Wilaya ya Mbozi hususan Jimbo la Mbozi Mashariki.

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Spika, kwanza namshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri na ya kutia matumaini, lakini pia naomba baada ya majibu hayo, niulize maswali mawili madogo ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, pamoja na nia nzuri ya Serikali ya kuendelea kupeleka mbolea ya ruzuku kwa wananchi, lakini bado bei ya mbolea hizi ni kubwa sana hasa ukizingatia kwamba wananchi wengi wa Tanzania bado ni maskini, uwezo wao ni mdogo. Kwa mfano, mbolea ya DAP bei yake ya soko ni karibu Sh. 65,000/= lakini ikiwa na ruzuku ya Serikali mwananchi huyo analazimika kulipia karibu kati Sh. 40,000/= au Sh. 45,000/=. Je, Serikali itakubaliana na mimi kwamba kuna umuhimu wa Serikali kuendelea kupunguza au kuweka ruzuku zaidi kwenye mbolea hii ili wananchi wengi waweze kuipata na kwa maana hiyo waweze kulima zaidi? (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, ziko habari kwamba mbolea ya Minjingu ambayo niliikataa Bungeni humu katika Bunge la Tisa kwamba haiwafai wananchi wa Mbozi kwa sababu iliharibu mazao yao. Sasa inaendelea kupelekwa tena kwa wananchi kwa ajili ya matumizi wakati utafiti haujafanyika. Serikali inasema nini kuhusu jambo hili? Ahsante.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Zambi kwamba bei ni kubwa lakini pia Serikali inaendelea kufanya jitihada kupunguza makali haya na ushahidi upo. Tulipoanza ruzuku ya mbolea huko nyuma kwenye miakaya 2003/2004 tulianza na shilingi bilioni mbili katika Mikoa minne ile *Big Four*, lakini tumeendelea kupandisha bajeti mwaka hadi na mwaka huu tumetoa shilingi bilioni 143.

Mheshimiwa Spika, huu ni ushahidi kwamba Serikali inalitambua hili na tutaendelea kupunguza makali haya kulingana na jinsi fedha tunazozipata. Lakini kimsingi nakubaliana naye na Serikali inaendelea kulitizama hili kila inapowezekana.

Mheshimiwa Spika, la pili, kuhusu mbolea ya Minjingu, naomba njibu namna hii, kwamba mbolea ya Minjingu tungependa tuitizame kama sisi tunavyojitizama wenywewe.

Mheshimiwa Spika, mbolea ya Minjingu ni mbolea ambayo kwanza ni ya asilia halafu ilikuwa haitumiki hapa, lakini ina tatizo moja kwamba yenyewe ina tabia ya kutumika vizuri zaidi mwaka unaofuata. Sasa kwa kweli wakulima kama walivyo watu wengine, wewe Mbunge *horizon* yako ni uchaguzi ujao, mfanyabiashara *horizon* yake ni mauzo ya leo kama yuko sokoni. Lakini mkulima naye *horizon* yake ni msimu ujao. Sasa anapoona mbolea hii *effect* yake ni msimu mwagine anakata tama, lakini kimsingi mbolea hii ni nzuri, kwanza ni ya asilia, inapatikana, haina madhara yoyote kwa sababu haina *chemicals*. Tumelichukua hili, wataalam katika Wizara ya Kilimo wanaendelea kufanya utafiti ili kuhakiki maeneo udongo unaofaa kwa mbolea hii ya Minjingu na dozi zinazofaa.

Mheshimiwa Spika, nalichukua hili kwamba wataalam wanalfanyia kazi na nina hakika baadaye tutatoa taarifa vizuri namna ya kuitumia mbolea hii ili wakulima wetu waitumie maana inapatikana nchini.

**MHE. MCH. LUCKSON N. MWANJALE:** Mheshimiwa Spika, nami nakushukuru. Naomba niulize swalı moja la nyongeza. Kwa kuwa mbolea hii mwaka jana pembejeo ilikuwa ni *package* nzima iliyogharimu Sh. 17,000/= na mwaka huu ni Sh. 40,000/=, nini kinachopelekea kupandisha bei mara mbili ya bei ya mwaka jana ambayo wananchi walikuwa wamepata kama sehemu ya ruzuku?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Spika, ninaomba niseme tu kwa kifupi kwamba mabadiliko ya bei zote hapa nchini iwe ya mbolea, iwe ya bidhaa nyingine zozote yanatokana na gharama za usafirishaji, gharama za ununuzi, mpaka kuifikisha kule. Kwa hiyo, hata mwaka ujao usitarajie kwamba itakuwa hivyo hivyo, inawezekana mbolea hiyo ikawa tofauti kulingana na gharama zitakavyokuwa zimebadilika hapa nchini. Kwa hiyo, kimsingi sidhani kama bei ya mwaka huu itakuwa hiyo na mwaka ujao itakuwa hiyo, haiwezekani. Hata kwenye bidhaa nyingine kuna tofauti inajitokeza.

Na. 88

#### **Ruzuku Kwenye Zao la Tumbaku**

**MHE. VITA R. KAWAWA (K.n.y MHE. VICTOR K. MWAMBALASWA)** aliuliza:-

Serikali imefanya kazi nzuri sana ya kuweka ruzuku kwenye pembejeo za mazao ya chakula na baada ya kuona mafanikio ya kazi hiyo, Serikali imeendeleza ruzuku hiyo kwenye mazao ya biashara ikianzia na pamba:-

- (a) Je, Serikali iko tayari kuendeleza kazi hii nzuri kwenye zao la Tumbaku msimu wa kilimo ujao?
- (b) Je, Serikali ina mpango gani wa kuwaelimisha mawakala wa pembejeo ambao kwa kasi kidogo wanatia dosari kazi hii nzuri?

## **NAIBU WAZIRI WA KILIMO CHAKULA NA USHIRIKA alijibu:-**

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika napenda kujibu swali la Mheshimiwa Victor Kilasile Mwambalaswa, Mbunge wa Lupa, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali itaendeleza kazi ya kutoa ruzuku kwa mazao yaliyopewa ruzuku katika msimu uliopita na kuendelea kuongeza idadi ya mazao yanayopata ruzuku ya pembejeo (likiwemo zao la tumbaku) kadri uwezo wa kifedha utakavyoruhusu kuititia bajeti yake ya mwaka 2011/2012 na miaka ijayo.

Mheshimiwa Spika, mchango wa Bodi ya Mazao, Mashirika yasiyo ya kiserikali na Kampuni mbalimbali ambazo zimeonyesha bidii ya kuwawezesha wakulima kuzalisha kwa tija zinaungwa mkono na kuendelea kutegemewa.

(b) Hivi sasa Serikali inatekeleza mpango wa kutoa mafunzo kwa mawakala pembejeo nchini. Kazi hiyo, inafanyika kwa kushirikiana na taasisi ijulikanayo kama *Citizen Network for Foreign Affairs*. Mafunzo hayo, yanahusu mbinu za biashara na maadili yake pamoja na matumizi ya hifadhi salama ya pembejeo za kilimo. Tangu yalipoanza mwaka 2008/2009, jumla ya mawakala wa pembejeo za kilimo 2,702 wamepatiwa mafunzo kutoka katika Halmashauri 53 za Mikoa ya Arusha, Kilimanjaro, Morogoro, Iringa, Mbeya, Ruvuma, Rukwa, Kigoma, Mara, Mwanza, Shinyanga, Manyara, Tabora na Tanga. Utaratibu huu wa kutoa mafunzo kwa mawakala unaendelea kutekelezwa kila mwaka hadi mawakala wote nchini watakapokuwa wamepatiwa mafunzo husika.

**MHE. VITA R. KAWAWA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa fursa ya kuuliza swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa, zao hili la Tumbaku limedhihirisha ni chanzo muhimu sana kwa pato la Taifa, kwanza kwa kuliingizia dola za Kimarekani milioni 127.3 mwaka jana na kuiingizia Serikali kodi za ndani shilingi bilioni 98, lakini pia kuingizia Halmashauri zetu shilingi bilioni 13: Je, Serikali kwa umuhimu huo inaweza kuingiza zao hili kuanzia msimu ujao wakulima kupata ruzuku ili waweze kuzalisha zaidi na kuweza kuongezea pato la Taifa na kukuza uchumi wetu?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Spika, Kama nilivyosema katika majibu yangu ya swali la msingi, zao la Tumbaku tunaliangalia kama mazao mengine, tunaifikiria pia kuliwekea ruzuku na pamoja na hayo, nadhani pia ni muhimu nimfahamishe Mheshimiwa Vita Kawawa kwamba uzalishaji ambao umefanywa na wakulima katika msimu huu, sisi tumeutambua na tunatambua hata kilio chao kwamba wamezalisha hata ziada ambayo bado inaelekea kukosa soko na hivi sasa tunajipanga sisi kama Serikali kusaidia wakulima kutafuta masoko hata nje ya nchi ili ziada ile ambayo imezalishwa ipate soko, vinginevyo, inawezekana tena mwaka mwingine uzalishaji ukapungua.

**MHE. CYNTHIA HILDA NGOYE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi. Ninaomba kuuliza swali moja dogo tu la nyongeza.

Kwa kuwa, uzalishaji wa mazao haya ya biashara mengi sana umerudi nyuma na hasa mazao kama Kahawa na Pamba na ni mazao ambayo kwa ujumla wake yanatuungezea sana uchumi katika nchi yetu. Je, Serikali haioni kwamba sasa kuna umuhimu wa kujipanga upya iweze kufikiria sasa kuweka ruzuku ya kutosha kwa mazao haya ili kuchochea moyo wa wananchi waweze kuzalisha mazao haya kwa wingi?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua kabisa umuhimu wa mazao haya ya biashara yote na mchango wake katika uingizaji wa mapato ya Serikali hasa kwenye fedha za kigeni na ndiyo maana tunaendelea kutoa na nimesema katika majibu ya awali kwamba tunaendelea kuongeza fedha za ruzuku mwaka hadi mwaka. Nimesema tulianza na shilingi bilioni mbili huko nyuma mwaka huo, tumefika shilingi bilioni 143 na jinsi fedha zitakavyokuwa zinapatikana tutaongeza.

Hata hivyo, napenda nimwarifu Mheshimiwa Cynthia H. Ngoye kwamba katika msimu huu tumetumia utaratibu wa vocha kwa mazao ya chakula, lakini pia tumetumia utaratibu nje ya vocha kutoa ruzuku kwa ajili ya mbegu za Chai na Kahawa. Kwa hiyo, tutaendelea kuyaangalia mazao haya yote bila kuyabagua kwa sababu yote yana mchango muhimu.

Na. 89

#### **Kuchelewa Kuanza kwa Mradi wa Ukarabati wa Bandari Kigoma**

**MHE. MHONGA S. RUHWANYA (K.n.y. MHE. KABWE Z. ZITTO)**  
aliuliza:-

Kwanini Serikali imechelewa kuanza mradi wa ukarabati wa Bandari ya Kigoma kupitia ufadhili wa Shirika la *JICA* la Japan?

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI alijibu:-**

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Kabwe Zuberi Zitto, Mbunge wa Kigoma Kaskazini, kama ifuatavyo:-

Serikali inatambua umuhimu wa Bandari ya Kigoma na imekuwa ikitafuta fedha kutoka kwa wafadhili mbalimbali ikiwa ni pamoja na shirika la *JICA* la Japan kwa ajili ya ukarabati wa bandari hiyo. Baada ya tathmini Serikali iliwakilisha maombi ya dola za Kimarekani milioni 10 kwa *JICA* baada ya kuwa limeonyesha nia ya kugharamia mradi huu.

Mheshimiwa Spika, Shirika la *JICA* baada ya kupokea maombi yetu lilipendekeza kuwa ili kuboresha ufanisi wa utendaji wa bandari pamoja na ukarabati wa bandari, ni vyema miundombinu inayohudumia na kuzunguka bandari kama vile Reli na Barabara vikaboreshw. Kwa mantiki hii mfadhili aliona kuwa kuna haja ya kufanya tathmini ya mahitaji halisi ya ukarabati wa bandari na miundombinu hiyo. Hiyo ndiyo sababu iliyosababisha kuchelewa kuanza kwa mradi huu.

Mheshimiwa Spika, napenda kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa timu ya wataalam wawili kutoka *JICA* Tokyo, Japan na mmoja wa *JICA* Tanzania imeelekea Kigoma kwa ajili ya kukusanya taarifa muhimu za ukarabati wa bandari hiyo. Kwa taarifa kutoka Ubalozi wa Japani, timu hiyo ya wataalam itawasilisha ripoti yao kwa Balozi siku ya Ijumaa tarehe 18 Februari, 2011 tayari kwa hatua zaidi.

Ni matarajio ya Serikali kuwa ripoti ya utafiti huu mara itakapokamilika, itabainisha mahitaji halisi na kuharakisha upatikanaji wa fedha kwa ajili ya ukarabati wa bandari hiyo. Baada ya Serikali kuipokea ripoti ya *JICA*, tutakaa nao ili kuona ni kwa jinsi gani kazi hii inaanza mapema iwezekanavyo.

**MHE. MHONGA SAID RUHWANYA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali madogo mawili ya nyongeza.

Kuna taarifa kwamba tayari *JICA* walishafanya hiyo tathmini na dola milioni 23 zimeshatolewa. Je, ujenzi huo utaanza lini?

Lakini vilevile napenda kujua: Kwa nini ujenzi wa bandari ndogo ya Kagunga mpakani mwa Tanzania na Burundi unasuasua? Ahsante.

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Mhonga kwa maswali yaliyo *direct*. Mheshimiwa Naibu Waziri majibu tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Spika, ujenzi utaanza mara baada ya tathmini, nami wiki iliyopita niliongea na Balozi wa Japan akasema anasubiri taarifa hiyo, kuna *study* iliyofanywa kabla ya hapo, lakini waliongeza tathmini ya barabara pamoja na reli ambazo zinazunguka bandari wakaona miundombinu hiyo ni muhimu ili ifanyiwe kazi na iongezwe kwenye upembuzi huu na pesa ziweze kuongezwa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Bandari ya Kabunga, hilo nimelipokea na tutalifanyia kazi bila wasiwasi.

**SPIKA:** Ahsante. Hili swali ni la Kigoma, kwa hiyo Mheshimiwa David Z. Kafulila swali lingine la nyongeza.

**MHE. DAVID Z. KAFULILA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Waziri amezungumza kwamba ukarabati huu wa bandari unategemea sana na pengine unakwenda sambamba na huduma ya reli, na kwa muda mrefu Serikali imekuwa ikitoa ahadi za uboreshaji wa huduma ya reli pasipo mafanikio yoyote mpaka sasa reli ya kati ndiyo reli ya pili kwa uduni katika Bara la Afrika.

Mheshimiwa Naibu Waziri unatuambia nini? Ni lini huduma hii ya reli inaweza ikarejea japo kwa kiwango cha ile miaka ya 1990?

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Spika, katika maelezo yangu, reli niliyozungumzia ni reli inayozunguka bandari pamoja na barabara, lakini suala la Reli ya Kati ni suala la msingi. Mheshimiwa Waziri juzi alipokuwa anatoa taarifa yake ya Wizara ni kwamba tunahitaji mara moja shilingi bilioni 63 ili kuimarisha reli ya kati na tuna mpango wa kati, mpango wa muda mrefu kuboresha siyo reli tu ya kati, lakini tuna reli ya Tanga mpaka Musoma, reli ya kutoka Manyoni mpaka Singida, reli ya kutoka Mtwara mpaka Mchuchuma na Liganga na pia tuna reli ya *TAZARA*. Hizo zote ziko katika mpango wetu na Ilani ya Uchaguzi ya Chama Tawala ili kuboresha miundombinu ya reli na bandari pamoja na viwanja vya ndege.

Na. 90

### **Utaratibu wa Kulipa Kivuko kwa Wiki au Mwezi**

**MHE. PINDI H. CHANA** aliuliza:-

Wananchi wanaotumia kivuko cha Feri jijini Dar es Salaam hulipa nauli wao pamoja na magari kila wanapovuka: Je, ina mpango gani wa kuanzisha utaratibu wa kulipa usafiri kwa wiki au mwezi kwa watu pamoja na magari yao?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Pindi Hazara Chana Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, utaratibu wa kulipia usafiri kwa mwezi tuliuanzisha kwa majaribio mwezi Agosti, 2008 katika kivuko kwa magari ya taasisi chache zilizoomba kama ifuatavyo:-

Magari ya miradi ambayo inasaidiwa na washirika wa Maendeleo, magari ya kuchukua wanafunzi, magari ya mashirika ya umma, magari ya Mabalозi na Benki binafsi.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, utaratibu wa kutumia tiketi za msimu umeibua changamoto kadhaa za udhibiti wa abiria na mapato, hivyo kuilazimu Serikali ifikirie njia mpya ya uhakika zaidi. Tayari Wizara kupitia Wakala wake, *TEMESA*, imempata Mhandisi Mshauri Mwelekezi chini ya ufadhili wa Benki ya Dunia atakayesanifu mfumo muafaka wa kutumia mashine maalum ya kukatisha tiketi (*vending machine*). Mfumo huo

utawezesha tiketi za msimu (wiki au mwezi) kukatwa kirahisi na kwa haraka kwa kutumia mashine ambazo zitakuwa sehemu mbalimbali jijini ili kuondoa msongamano sehemu za kupandia na utarahisisha uwekaji wa kumbukumbu za makusanyo pamoja na udhibiti wa mapato. Kwa utaratibu wa mfumo huu, bandarini patakuwa ni sehemu ya kupandia au kuteremkia tu, siyo kuuzia tiketi. Aidha, sehemu za kupandia kutakuwa na mashine maalum za udhibiti zitakazoruhusu abiria wale tu wenye tiketi halali kuingia chomboni. Kazi ya usanifu inatarajiwa kukamilika mwezi Juni, 2011 na baada ya hapo utaratibu wa kumpata mzabuni wa kuleta mashine hizi utanza.

**MHE. PINDI H. CHANA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri sana ya Mheshimiwa Naibu Waziri na kwa kuwa utaratibu huu ni muhimu ambao unawawezesha wananchi kupanga bajeti yao na kulipa kwa wiki au mwezi na hata kwa mwaka, kwa mfano Uingereza na ni utaratibu unaotumika na nchi zilizoendelea: Naibu Waziri atakuwa tayari kutuhakikishia na kulisimamia jambo hili ili angalau *by June*, 2011 kama alivyoahidi jambo hili likaanza kufanya kazi?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, naomba nimuhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Mhandisi Mshauri Mwelekezi tuliyemteua ni Kampuni ya Kiholanzi iitwayo *Royal Hasconing* ambayo inaanza kazi hii katikati ya mwezi ujao na itakamilika kama nilivyosema kwenye jibu langu la msingi mwezi Julai mwaka huu.

**MHE. FAIDA MOHAMED BAKAR:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipatia nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa suluhisho la eneo lile siyo Feri bali ni kujengewa daraja wananchi wa maeneo yale: Je, Serikali ina mkakati gani wa makusudi na wa haraka wa kuwajengea daraja watu wa eneo lile?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Faida Mohamed Bakar kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, tayari kuna mpango ambao baadaye ukishaanza kukamilika tutalitaarifu Bunge lako Tukufu juu ya ujenzi wa daraja kati ya Kigamboni na Kivukoni. Mipango imefikia hatua nzuri. Lakini wakati tunasubiri mpango wa daraja, tutaendelea kuviimarisha vivuko vyetu vya Feri kati ya Kivukoni na Kigamboni.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

Na. 91

### **Kero ya Suala la Mirathi na Mafao ya Wastaafu**

**MHE. JOHN J. MNYIKA (K.n.y. MHE. SAID AMOUR ARFI)** aliuliza:-

Suala la upatikanaji wa mafao ya wastaafu na mambo yanayohusiana na mirathi kwa watumishi waliokufa kazini yamekuwa ni kero kubwa sana:-

Je, ni lini Serikali itaondoa kero hizi za muda mrefu ili wastaafu walipwe mafao yao mara wanapostaafu na mirathi kutolewa kwa wakati bila usumbufu kama ambao wanaupata sasa?

### **NAIBU WAZIRI WA FEDHA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa ruhusa yako napenda kujibu swali la Mheshimiwa Said Amour Arfi, Mbunge wa Mpanda Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kabisa anavyosema Mheshimiwa Mbunge, ucheleweshaji wa kupata mafao ya wastaafu na mambo nayaohusiana na mirathi kwa watumishi waliokufa kazini umekuwa ni mzigo usio wa lazima kwa wastaafu.

Mheshimiwa Spika, mafao ya wastaafu na mirathi ya watumishi wa Serikali Kuu na wale wa Serikali za Mitaa waliokufa kazini yanasmamiwa na Mifuko mitano ambayo ni Mfuko wa Pensheni kwa Watumishi wa Umma (*PSPF*), mfuko wa Pensheni kwa Watumishi wa Serikali za Mitaa (*LAPF*), Mfuko wa Pensheni wa Mashirika ya Umma (*PPF*), Mfuko wa Akiba na Watumishi wa Serikali (*GEPF*) na Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (*NSSF*).

Mheshimiwa Spika, hii mifuko ni mahususi kwa malipo ya mafao na mirathi kwa wastaafu na watumishi waliokufa kazini kulingana na stahili zao. Mifuko hii ya pensheni ndiyo inayowajibika kutoa malipo stahili kwa wakati. Mchakato wa malipo huanzia kwa mwajiri ambaye huandaa nyaraka za madai ya malipo na kuziwasilisha kwenye mfuko husika. Mifuko huzipatia nyaraka na kukokotoa kiasi cha malipo na kisha kupeleka hundi kwa walengwa.

Mheshimiwa Spika, ucheleweshaji wa maandalizi ya mafao pamoja na mambo mengine yanayotokana na utunzaji wa kumbukumbu na mawasiliano hafifu kwa upande wa mifuko. Hii inajumuisha malumbano ya kifamilia kuhusu uteuzi wa msimamizi wa mirathi husika.

Mheshimiwa Spika, endapo kumbukumbu za mstaafu zitakuwa kamilifu na michango yote itakuwa ikiwasilishwa katika mfuko kama inavyotakiwa, mstaafu atawea kupokea malipo yake ya kustaafu mara anapostaafu bila usumbufu usio wa lazima.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa mirathi, suala la utmilifu wa kumbukumbu zote za utumishi, pia makubaliano ya kifamilia kuhusu uteuzi wa msimamizi wa mirathi hiyo ni muhimu sana. Kwa hiyo, endapo kutakuwa na kumbukumbu zinazotakiwa pia na nyaraka zote za mirathi zitakuwa zimewasilishwa kama inavyotakiwa, warithi wataweza kulipwa mirathi yao kwa haraka na bila usumbufu wowote.

**MHE. JOHN. J. MNYIKA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri nina maswali ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Moja, kwa kuwa Mheshimiwa Naibu Waziri amesema kwamba moja ya sababu zinazochangia kuchelewesha mafao na mirathi ni matatizo ya mawasiliano ambayo mengine yanahusisha wahusika na mengine yanahusisha mifuko. Je, ni lini Serikali itaboresha huu mfumo wa mawasiliano? Kwa sababu kwa mujibu wa taarifa tunazopokea kwa wananchi ni kwamba wapo wananchi ambao wamepeleka taarifa zao zote, lakini bado wanalamika kuhusiana na kupata mafao ama mirathi kwa wakati.

Pili, Mheshimiwa Naibu Waziri katika majibu yake amezungumzia wastaifu na wanaohusika na mirathi ambao wanahudumiwa na ile mifuko mitano. Je, Serikali inatoa tamko gani kwa wastaifu ambao hawahudumiwi na ile mifuko kama wastaifu wa Jumuiya ya Afrika Mashariki ambao na wenyewe kwa muda mrefu sana wanalamika kuhusu mafao yao na masuala mengine yanahohusiana na mirathi?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Spika, suala la *pension* na mirathi linahusisha Taasisi tofauti. Kwanza, linamhusu mfanyakazi au Marehemu; pili, linamhusu mwajiri wake; tatu, linamhusu Mahakama kwa upande wa mirathi; na nne, linamhusu Hazina au Mfuko. Tatizo la kuchelewesha mara nyingi linatokea iwapo mmoja katika hawa hawakutekeleza wajibu wake kwa wakati na ipasavyo. Inawezekana mwajiri kapeleka kumbukumbu lakini zikawa hazikutumia au zina kasoro, kwa hiyo, zikienda kufanyiwa kazi zinarudishwa tena. Kwa hiyo, kile kipindi cha mzunguko ndiyo kinasababisha kuleta matatizo.

Kwa upande wa mirathi, jambo muhimu linalotakiwa ni nani anasimamia, sasa tuna mila ambazo zinafanya hili jambo liwe gumu na la kuchelewa. Hatukubaliani kirahisi kwenye familia nani anasimamia na kuna mizengwe ambayo iko mingi. Kitu ambacho tunaweza kusema ni kwamba tunakumbushana mara nyingi kwamba kila mtu atimize wajibu wake na kwa upande mwingine tunawashauri Watanzania waliangalie suala la kuandika wosia wakati Magharibi ikifika.

Mheshimiwa Spika, kuhusu wastaifu wa Afrika Mashariki, suala hili limekwenda Mahakama Kuu na likaenda Mahakama ya Rufaa. Uamuzi wa Mahakama ya Rufaa ulikuwa kwamba hili suala litafutiwe Jaji mwingine wa kuliendeleza na kwa sababu hiyo, hatuna cha kusema mpaka Jaji ateuliwe na hatua za kulishughulikia lifanyike na tupewe maelekezo.

**SPIKA:** Kwa hiyo, kwa maana nyingine liko Mahakamani. Tunaendelea na Wizara ya Elimu, Mafunzo na Ufundu, Mheshimiwa Rose.

## KUHUSU UTARATIBU

**SPIKA:** Utaratibu kwenye maswali? Hapana, naomba tuendelee. Mheshimiwa Rose Kamili Sukum.

**Uwiano wa Wanafunzi wa Kike na Kiume Kujiunga na  
Sekondari na Vuyo vya Juu**

**MHE. CHRISTOWAJA G. MTINDA (k.n.y. MHE. ROSE KAMILI SUKUM)** aliuliza:-

Uwiano kati ya wanafunzi wa kike na kiume kujiunga na sekondari na vuyo hapa nchini umepungua kutoka ngazi ya chini kwenda ngazi ya juu, ambapo kwa miaka mitano nyuma wanafunzi walioandikishwa shule kwa shule za msingi ulikuwa ni asilimia 50, wa kiume na asilimia 50 wa kike. Sekondari uwiano ulikuwa asilimia 55.5 wa kiume na asilimia 45.5 wa kike wakati Elimu ya juu ni asilimia 64.7 wa kiume na asilimia 35.3 wa kike.

- (a) Je, ni sababu gani zimefanya mpaka sasa kuwepo kwa tofauti ya uwiano mkubwa namna hiyo mionganoni mwa wanafunzi wa kike na wa kiume katika ngazi ya Elimu ya Juu?
- (b) Je, Serikali ina mikakati gani mahususi ya kuondoa tofauti hiyo kubwa ya uwiano wa kijinsia unaoendelea kulikumba Taifa katika ngazi ya Elimu ya Juu?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Rose Kamili Sukum, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, uwiano katika shule za Sekondari katika kipindi cha miaka mitano iliyopita ulikuwa ni asilimia 53.3 wa kiume na asilimia 47.7 wa kike na katika ngazi ya Elimu ya Juu asilimia ya wanafunzi wa kiume ni 64.7 na wa kike ni asilimia 35.3.

Mheshimiwa Spika, wanafunzi katika Shule za Msingi na Sekondari wanakabiliwa na changamoto nyingi. Hata hivyo, wanafunzi wa kike wanakabiliwa na changamoto mahususi zikiwemo za baadhi ya wazazi kutoona umuhimu wa elimu kwa watoto kike, baadhi ya wazazi kuwalazimisha kuolewa, kupata mimba, ukosefu wa hosteli na udhaifu katika uendeshaji wa baadhi ya hosteli na wanafunzi wa kike kupewa majukumu ya nyumbani yakiwemo ya kupika, kufua na kulea watoto.

Mheshimiwa Spika, Serikali inachukua hatua za dhati kuondoa tofauti ya uwiano wa kijinsia katika ngazi ya Elimu ya Juu kwa kufanya yafuatayo:-

- (1) Kushirikiana na wadau wa elimu kujenga hosteli za wasichana katika ngazi zote za elimu ili kuwapa mazingira bora ya kujifunzia;
- (2) Kuwapa maandalizi ya awali wasichana (*pre-entry programmes*) wakati wanajiunga na Elimu ya Juu kwa *programme* ya Sayansi. Huu ni utaratibu wa kuwapa mafunzo ya awali ya muda mfupi wanafunzi wa kike ili kuwaweka sawa kukabiliana na programu rasmi za masomo wakati mwaka mpya wa masomo unapoanza.
- (3) Kuwachukulia hatua za kisheria wanaume wote wanaohusika kuwapa mimba au kuwaoa wanafunzi wa kike, lakini vilevile kuwachukulia hatua za kisheria wazazi wanaowaoza watoto wao kabla hawajamaliza masomo yao.

**MHE. CHRISTOWAJA G. MTINDA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Pamoja na majibu ya Mheshimiwa Waziri, nina swali dogo la nyongeza.

Pamoja na nia njema ya Serikali ya kuwapa mafunzo ya awali watoto wa kike *pre entry programmes* katika Vyuo Vikuu, Serikali sasa haioni kuna umuhimu wa kujenga maabara katika shule zote za sekondari zikiwemo za Kata, pia kuimarisha na kuongeza vifaa katika zile sekondari ambazo zilikuwa na maabara tangu awali ili wanafunzi wa kike pamoja na wa kiume wanapokwenda Vyuo Vikuu wawe wameshaanza kufanya mazoezi ya kisayansi wakiwa tangu Shule za Sekondari?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Spika, nadhani juzi wakati natoa majumuisho ya Wizara yangu ya Elimu nilisema kuna mpango mkakati wa Wizara ama Serikali wa MESS ambaao tunafadhiliwa. Ndani ya *programme* za mpango wa MESS kuna mpango mahususi wa kujenga maabara moja katika shule zetu hizi za ngazi ya Kata. Kwa hiyo, nadhani baada ya kufanya hivyo, watoto wengi watapata masomo ya Sayansi kwa mfumo wa vitendo.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

Na. 93

#### **Kuanza Rasmi Kidato cha Tano katika Shule za Mpitimbi na Mabada Day – Peramiho**

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA** aliuliza:-

Vigezo vyote vya uanzishaji Kidato cha Tano na Sita katika Shule za Sekondari za Mpitimbi na *Madaba Day* vimekamilika na Wakaguzi waliishamaliza kazi zao.

Je, ni lini Serikali itapeleka walimu na wanafunzi ili shule hizo zianze rasmi?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Jenista J. Mhagama, Mbunge wa Peramiho, kama ifuatavyo:-

Utaratibu ni kwamba shule yoyote ikitimiza vigezo muhimu vilivyowekwa na Ofisi ya Kamishina wa Elimu inaruhusiwa kuanzisha Kidato cha Tano. Hata hivyo, utimilifu wa vigezo hivi inabidi kuhakikiwa na Ofisi ya Ukaguzi wa Shule Kanda.

Mheshimiwa Spika, mnamo mwezi Desemba, 2010 Wizara yangu ilitembelea Mkoa wa Ruvuma kwa nia ya kukagua uwezekano wa kuanzisha Kidato cha Tano katika Shule za Sekondari za *Madaba Day* na Mpitimbi. Katika ukaguzi wake ilibainika baadhi ya mapungufu na taarifa ilikabidhiwa kwa Katibu Tawala Mkoa wa Ruvuma na akatoa ushauri kwamba mapungufu hayo yatarekebishwa. Aidha, Mkaguzi Mkuu wa Shule Kanda ya Nyanda za Juu Kusini amekagua shule hizo na kutoa mapendekezo kwa Kamishina wa Elimu.

Mheshimiwa Spika, napenda kumtaarifu Mheshimiwa Mbunge, kwamba Sekondari ya *Mabada Day* imetimiza vigezo na kuruhusiwa kuanzishwa mkondo mmoja wa *HKL*. Hivyo mwaka huu watapelekwa wanafunzi. Aidha, Shule ya Sekondari Mpitimbi bado haijakamilisha vigezo. Pindi itakapokamilisha itaruhusiwa kuanzisha Kidato cha Tano.

Mheshimiwa Spika, Walimu wa Shahada wamepangwa tayari katika Halmashauri ya Songea Vijijini, mwezi Januari, 2011.

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa ruhusa ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa wananchi wa Kata ya Mpitimbi kwa kuzingatia mfano bora wa kimaendeleo wa elimu uliopo katika Kata ya Maposeni; na kwa kuwa na shule ya kidato cha tano bado na wao wana azma kubwa ya kuwa na sekondari hiyo ya kidato cha tano; na kwa kuwa tayari wameyagundua mapungufu hayo na wako tayari kabisa kuyatekeleza na kuyaondoa:

Je, Mheshimiwa Naibu Waziri yuko tayari kuniahidi mimi na wananchi wa Jimbo la Peramiho kupitia Kata hiyo kwamba mara baada ya mapungufu hayo kutekelezeka shule hiyo nayo ifunguliwe haraka kadri iwezekanavyo?

Lakini swali la pili ni kwamba ninafahamu kabisa wananchi wa Madaba wamefarijika na kuwa na furaha kubwa baada ya kusikia kwamba mwaka huu shule ile itapokea wanafunzi wa kidato cha tano kwa maendeleo ya elimu katika Jimbo letu na Mheshimiwa Waziri ameahidi kwamba walimu watapelekwa kwa muda unaotakiwa.

Je, Mheshimiwa Waziri yuko tayari kushirikiana na mimi na kuhakikisha kwamba kwa pamoja tunajua idadi ya Walimu watakokwenda kuanzisha shule ile na watakwenda kwa wakati unaotakiwa?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Spika, kwanza, kuhusu shule ya Madaba ambayo sasa tayari Serikali imesharidhia kwamba wapatiwe mkondo wa *A-level*, nina hakika wakaguzi walipofika pale baada ya kubaini kwamba kulikuwa na upungufu, lakini yale ambayo ni ya msingi, lakini mengine bado tulishauri kwamba waendelee kuyakamilisha pamoja na kumalizia nyumba.

Kwa hiyo, nina hakika kabisa kwamba Wizara kwa sababu imeridhia namhakikishia Mheshimiwa Jenista Mhagama kwamba walimu watakwenda pale kwa ajili ya masomo ya Historia, Kiswahili na *Language*.

Mheshimiwa Spika, lakini vilevile napenda sana kumpongeza Mheshimiwa Jenista Mhagama kwa kufuatilia masuala ya elimu katika Jimbo lake kwa sababu hata katika taarifa za ukaguzi inaonekana alichangia mchango mkubwa sana mpaka hizi shule kuweza kuanzishwa na sasa hivi wanataka ziwe “A” *level*.

Namhakikishia kabisa kwamba Serikali haina tatizo kama Mpitimbi wakikamilisha vigezo ambavyo ukaguzi waliona ni mapungufu, sisi tuko tayari wakati wowote, Wizara iko tayari kuanzisha kidato cha tano wakati wowote. Kwa hiyo, naomba yale mapungufu wayakamilishe.

Na. 94

### **Kufungua Mgodi wa Makaa ya Mawe Kiwira**

**MHE. KIBONA A. NIKUSUMA** aliuliza:-

Tangu Mgodi wa Makaa ya Mawe wa Kiwira usitishe shughuli za uzalishaji, Wananchi zaidi ya mia nane pamoja na familia zao wamekosa ajira na kufanya maisha yao kuwa magumu sana, pamoja na Wilaya za jirani za Kyela na Rungwe nao wameathiriwa na kusita kwa shughuli katika Mgodi huo na kushindwa hata kujikimu maisha yao na kusomesha watoto wao:-

Je, ni lini Serikali itafungua Mgodi huo na kurejesha ajira kwa Watu wa Ileje na Wilaya za jirani waliokuwa wanategemea Mgodi huo?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Kibona A. Nikusuma, Mbunge wa Ileje, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Mgodi wa Kiwira ulibinafsishwa na kuwa chini ya umiliki wa Kampuni ya *Tan Power Resources Limited* mwaka 2007, baada ya uendeshaji wa Mgodi huo kukosa tija na ufanisi. Ubinafsishwaji huo ulilenga kuongeza uzalishaji wa makaa ya mawe na kupanua uwezo wa mtambo wa kuzalisha umeme kutoka MW 6 hadi kufikia MW 200. Ili kuweza kufikia kiwango hicho, Kamapuni ya *Tan Power Resources Limited* ilihitaji kupata kiasi cha Dola za Marekani 400,000. Pamoja na juhudzi za kupata

kiasi hicho, kampuni hiyo ilipata mkopo wa takriban shilingi bilioni 15.14 kutoka Taasisi za fedha za hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, kutokana na Kampuni ya *Tan Power Resources* kushindwa kuendesha Mgodi wa Kiwira kutokana na sababu mbalimbali ikiwemo ya kushindwa kupata mkopo mkubwa wa milioni 400, kiasi kilichohitajika mwaka 2009, Serikali iliamua kuuchukua tena Mgodi huo ili kumtafuta mbia mpya. Itakumbukwa kuwa, Mwezi Julai, 2009, Serikali ilibatilisha uamuzi wake wa kulifunga Shirika la Madini la Taifa (*STAMICO*) ili lisimamie maslahi ya Taifa katika Sekta ya Madini. Kwa sasa na kwa kuzingatia haya, Wizara yangu na Shirika la STAMICO kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha na Uchumi, iko katika mchakato wa kumpata mwekezaji mpya atakayeweza kuendesha Mgodi huo na kupata ufumbuzi wa suala la Wafanyakazi waliokosa ajira kutokana na kusimama kwa shughuli za Mgodi.

Mheshimiwa Spika, napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge na Bunge lako Tukufu kuwa, punde Mwekezaji huyo mpya atakapopatikana na Serikali kujiridhisha kwa ukamilifu, Mgodi huo utafunguliwa na ajira kwa Wananchi wa Ileje na Wilaya za jirani waliokuwa wanategemea Mgodi huo itarejea tena.

**MHE. KIBONA A. NIKUSUMA:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Wananchi wa Wilaya ya Ileje, Wilaya ya Kyela na Wilaya ya Rungwe walio wengi wameajiriwa na Kampuni ya Ulinzi inayoitwa *New Imara Security Card*; na kwa kuwa Wananchi hawa hawajalipwa mishahara yao tangu mwezi Julai mwaka jana, sababu kubwa ni Kampuni kutolipwa fedha kutoka Serikalini; na kwa kuwa Wananchi hawa wanateseka na mwajiri wao ametoa *notice* ya kusitisha ulinzi katika Mgodi ule mwisho tarehe 28 mwezi huu:-

(a) Je, Mheshimiwa Waziri yuko tayari kunihakikishia kwamba kampuni italipwa ili na wafanyakazi walipwe waendelee kulinda mali zetu?

(b) Kwa kuwa Vijiji vya Kapeta na London ni vijiji ambavyo vinazunguka Mgodi wa Makaa ya Mawe ya Kiwira tangu mwaka 1983 Mgodi ule ulipofunguliwa na baadaye umebin afsishwa kama Waziri alivyosema lakini Wananchi wale hawajanufaika na umeme ambao kampuni inazalisha, badala yake umeme ule umefaidisha watu wa mbali kinyume na sera ya uwekezaji ambapo tumesema wananchi wanaozunguka migodi au wanaoishi karibu na wawekezaji wafaidi kwanza. Je, Mheshimiwa Waziri atanihakikishia kwamba pindi Mgodi huu utakapofunguliwa vijiji hivi vitapewa kipaumbele namba moja kwa ajili ya kupata umeme? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu maswali ya Mheshimiwa Kibona, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, tarehe 11 Februari 2011, wakati Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini anajibu swali la Wafanyakazi wa Mgodi wa Kiwira alieleza kwamba, Serikali imekuwa ikikamilisha malipo hayo kwa awamu mbili na hili suala la wafanyakazi wa kampuni ya ulinzi hasa ukizingatia umuhimu wa kuwepo ulinzi kwa zile

rasilimali ambazo ziko pale tayari, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Kibona kwamba, Serikali inalifahamu na inalifanyia kazi na hili litapata ufumbuzi haraka iwezekanavyo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu swal la pili, wakati Mgodi unaanzishwa mwaka 1983, uzalishaji wenyewe wa umeme ulikuwa wa MW 6, sasa hivi makusudio ni makubwa sana na ndiyo maana tunasema na *STAMICO* wamo na watu wengine ambao tunakusudia kutoka pale kuja kwenye uzalishaji mwingine kabisa ambao unatarajiwa kupata MW 200. Kwa hakika kabisa, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Kibona kwamba, maeneo yote yaliyokuwepo pale jirani ambayo hayana umeme, yatanufaika na umeme ambao utazalishwa pale kwa sababu umeme wenyewe utakuwa ni mwingi sana kwa maeneo ya pale na matumizi ya Mradi wenyewe. (*Makofi*)

Na. 95

### **Kufikisha Umeme Vijijini**

**MHE. AMOS G. MAKALLA** aliuliza:-

Serikali imonesha nia ya dhati kufikisha umeme vijijini kwa kuanzisha Wakala wa Nishati Vijijini (*REA*) lakini licha ya nia hiyo nzuri, ni miaka Kumi na mitatu imepita tangu nguzo za umeme kwenda Tarafa ya Mgeta ziwekwe eneo la Peko Misegese bila kufikishwa Langali, Tarafa ya Mgeta:-

- (a) Je, Serikali inasema nini juu ya Mradi huo?
- (b) Je, ni lini sasa Mradi huo wa Umeme utafikishwa Kata ya Langati, Tarafa ya Mgeta?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swal la Mheshimiwa Amos G. Makalla, Mbunge wa Mvomero, lenye sehemu (a ) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Mradi wa Umeme katika Tarafa ya Mgeta ulianza kwa kufadhiliwa na TANESCO. Utekelezaji wa Mradi huu umechukua muda mrefu, kutokana na TANESCO kukosa fungu la kutekeleza Mradi huo kwa wakati kama ilivyokusudiwa. Hata hivyo, kwa hivi sasa Mradi huu utapata utekelezaji chini ya ufadhili wa *Millenium Challenge Corporation (MCC)*. Tayari Mkandarasi wa kutekeleza Mradi huo amepatikana na zoezi linaloendelea kwa sasa ni malipo kwa Wananchi ambao mali zao zitaathirika na Mradi kulingana na tathmini ya fidia iliyokwishafanyika.

Mheshimiwa Spika, malipo ya fidia kwa Mikoa yote sita iliyo chini ya ufadhili wa MCC, yanatarajiwaka kukamilika mwezi Mei, 2011. Utekelezaji wa Miradi hii kwa hatua inayofuata unatarajiwaka kuanza mwishoni mwa mwezi Mei, 2011 ikiwemo Mkoa wa Morogoro, Tarafa ya Mgeta. Mradi wa Umeme katika Kata ya Langati, Tarafa ya Mgeta, unatarajiwaka kukamilika mwezi Novemba, 2011.

Mheshimiwa Spika, namwomba Mheshimiwa Mbunge na Wabunge wengine wanaopitiwa na Miradi ya Usambazaji wa Umeme yenye Ufadhilli wa MCC, tuendelee kuwasilisna na kufanya kazi kwa ushirikiano wa karibu na Wizara yangu ili kufuatilia ukamilishaji wa Miradi hii.

**MHE. AMOS G. MAKALLA:** Mheshimiwa Spika, namshukuru Waziri kwa majibu mazuri, yanayotoa matumaini kwa Wananchi wa Mgeta kupata umeme. Pamoja na majibu mazuri, naomba kuuliza maswali kama ifuatavyo:-

- (a) Kwa kuwa mkandarasi ameshapatikana na ameshaeleza kwamba Wananchi hawa watapata umeme mwezi Novemba; je, anaweza akanitajia jina la mkandarasi anayefanya kazi hiyo sasa?
- (b) Kwa kuwa ameelleza kwamba sasa hivi wanakamilisha suala la fidia; je, anajua kwamba yapo manung'unico kuna wananchi ambao bado hawajapata fidia na wengine wamepunjwa fidia zao?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Makalla, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mkandarasi aliyepatikana kwa Mikoa, Mikoa yenewe ya MCC kama nilivyosema, kwa kipande hiki cha usambazaji wa umeme iko sita. Sasa kwa mikoa ukiwemo Mkoa wa Morogoro, Mkandarasi ni Simbion wa Marekani. Kwa huu Mkoa wa Dodoma ambao nao wana MCC kazi kama hiyo hiyo inafanywa na Mkandarasi aitwa Paic naye wa North Caroline kule Marekani. Kwa hiyo, Mkandarasi anayeshughulikia Miradi ya Morogoro ni Simbion Power ya Marekani.

Swali la pili, hili suala la fidia analosema kwa sasa hivi katika hatua yote kwa sababu miradi hii kwa mikoa yote sita inakwenda pamoja, sasa hivi tuko kwenye utekelezaji wa masuala ya fidia na malipo yake. Masuala ya malipo ya fidia yana namna mbili; kuna malipo ya fidia ya *Red Zone* na malipo ya fidia kwa *Green Zone*. *Red Zone* ni yale malipo ambayo unapofidia nyumba, kuna nyumba watu wanakaa inabidi iondoke sasa pale utaratibu wake ni tofauti kwa sababu ukishamlipa unampa miezi mitatu akatafute mazingira mengine. *Green Zone* ni pale ambapo kuna masuala ambayo siyo kwenye makazi ya nyumba. Kwa hiyo, nataka nimfahamishe Mheshimiwa Amos Makalla na ninamshukuru sana kwa sababu amefika Wizarani kufuatilia suala hili kwa karibu kwa niaba ya Wananchi wake wa Mvomero. Naomba nimfahamishe kwamba, pale ambapo matatizo haya ya ulipaji wa fidia yataendelea na hakuna matatizo yatakayojiri baada ya

hapo, ndiyo maana tumeweka kipindi hiki mpaka mwezi Mei, tunatarajia kwamba masuala haya yatakuwa yameshakamilika. Nakushukuru sana.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, maswali yamekwisha. Tuliongeza muda kwa sababu kulikuwa na uwasilishaji wa nyaraka halafu na Mheshimiwa Tundu Lissu alitaka kutoa hoja. Kwa hiyo, ndiyo maana tumeongeza huu muda ku-*cover* ule muda uliopotea.

Mheshimiwa Mkono, ulikuwa umeuliza kuhusu utaratibu?

### KUHUSU UTARATIBU

**MHE. NIMROD E. MKONO:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Wakati Mheshimiwa David Kafulila anauliza swali, alikuwa upande wa eneo ambalo Waheshimiwa Mawaziri wanakaa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Kafulila hakuondoka alikaa pale, Mheshimiwa Mnyika ndiyo alikuwa kule.

**MHE. NIMROD E. MKONO:** Je, inaruhusiwa kufanya hivyo; unatoka kwenye kiti chako unakwenda upande anakokaa Waziri ukaanza kuuliza swali ama kujibu?

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, siyo tatizo; tatizo kama ni *seat za opposition* ziko upande huu, sasa huyu alikwenda ku-*consult* na Mawaziri hapa, kwa hiyo, swali likamkuta yuko kule hakuna tatizo. Hajavunja kanuni yoyote, kama hivyo anavyofanya Mheshimiwa Tundu Lissu hajakosea. Ila mkiwa na uhakika kama ameshahamia CCM au vipi, hiyo ndiyo hamkuwa na uhakika; hakufanya kosa.

Waheshimiwa Wabunge, lingine, kabla sijatoa matangazo, nimeona kuna Mheshimiwa Mbunge mmoja simtaji jina, yeye kila akikosa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza anaandika kwa maandishi; swali la nyongeza kwa Mheshimiwa Waziri fulani. Wakati wa maswali huwezi kuandika maswali ya nyongeza maana yatajibowi lini sasa! Maswali ni ya papo kwa papo, kwa hiyo, ama umepata nafasi ya kuuliza swali kwa sauti au hukupata. Ukiandika maswali ya nyongeza ninaweza kumpa Waziri lakini atakujibu wapi; hatakjibui wala hawezi kukuandikia barua, kanuni haziruhusu kufanya hivyo. Kwa hiyo, naomba tu mridhike kwamba, siku hiyo ama uwe fundi wa kuandika maswali yako, ukiweza Spika akakuona bahati yako, asipokuona inakuwa bahati mbaya, lakini ukiandika hayaendi kokote.

Lingine, kuna Mheshimiwa nafikiri Conchesta Rwamlaza, alisema wakati nimempa nafasi Naibu Waziri kujibu swali lake wakati si Waziri aliyejikuwa anajibu, hakupata majibu ya swali lake.

Kuna njia mbili; moja ni wakati tumeahirisha Bunge unaweza kuuliza kwa maelezo binafsi kwamba, sikuridhishwa na majibu ya Waziri ama sikujibowi swali langu, basi unaweza kujieleza ukapata majibu yanayostahili. Lingine ni kwamba, Waziri mwenyewe anaweza kukujibu. Siku ile nadhani kosa lilikuwa la kwangu mimi, maana

nilimpa Waziri ambaye kwa kweli hakuwa anapaswa kujibu. Sasa mimi nilichukulia kwamba, kwa sababu mazingira yale anayafahamu, kumbe mtu akaeleza mambo yake mwenyewe. Nadhani nilikujibu siku ile ile kwa msingi huo.

Baada ya maelezo hayo, wageni walioko pale kwenye *gallery* mimi sijapewa majina, kwa hiyo, sitaki ku-risk kuwatambua hapa naweza kukosea. Kwa hiyo, mnakaribishwa wote.

Ninayo matangazo mengi kidogo; kwanza kabisa, mimi mwenyewe na Sekretarieti ya Tume ya Utumishi wa Bunge, tukimaliza kikao asubuhi hii, naomba tukutane kwenye *Board Room* ya Spika. Tume ambayo ilichaguliwa juzi hapa.

Matangazo mengine ni kwamba, Kamati za *LAAC*, *PAC* na *POAC*, naomba nitoe taarifa kwamba, hizi Kamati zote tatu wakutane kwenye mafunzo Dar es Salaam tarehe 20 mpaka 26. Wajumbe wa Kamati hizo mripoti Dar es Salaam tarehe 19 Februari, 2011. Zile Kamati za *PAC*, *POAC* na *LAAC*, Wenyeviti wao ni Mheshimiwa Augustino Mrema, Mheshimiwa John Cheyo na Makamu Mwenyekiti Mheshimiwa Deo Filikunjombe, *otherwise*, Mwenyekiti wake ni Zitto, wanawatangazia Wajumbe wake kwamba, mtakuwa na mafunzo kuanzia tarehe 20 – 26 Februari, 2011. Mafunzo haya ni utaratibu ambao *CAG* huwa anafanya, kuandaa hizi Kamati kabla hazijaanza kazi zao rasmi. Kwa hiyo, ni utaratibu rasmi kupitia Mradi wa *PFMR* ambao unafanya kazi hiyo. Nilikuta Kamati zingine wanasema na wao waingie katika Programu hii; nimewajibu kwamba, kabla ya Bunge la Aprili, Wabunge wote tutapata mafunzo au semina kupitia Kamishna wa Bajeti. Kwa sababu kila Kamati itabidi ipitie Bajeti za Wizara ambazo ziko chini yao. Kwa hiyo, mtapata mafunzo ya namna ya kupitia zile Bajeti za Wizara. Hawa wanakwenda kufundishwa namna ya kukagua hesabu zilizopita. Kwa hiyo, hamko sawa, maana nimeona wengine wanasema wanaomba na wao washiriki huko; ninyi mtashiriki kwa utaratibu mwengine. Kwa hiyo, naomba hili lieleweke.

Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Jamii, Mheshimiwa Jenista Mhagama, anaomba niwatangazie Wabunge wa Kamati hiyo kuwa, kutakuwa na Kikao cha Kamati leo mara baada ya kuahirisha Bunge kwenye Ukumbi wa Pius Msekwa; walikuwa wengi sana.

Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Fedha na Uchumi, Mheshimiwa Dkt. Abdallah Kigoda, anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Fedha na Uchumi kuwa, kutakuwa na Kikao cha Kamati mara baada ya kuahirisha kikao hiki. Kikao hiki kitafanyika Ukumbi Namba 219. Wajumbe wake wanaombwa kuhudhuria.

Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala, Mheshimiwa Pindi Chana, ye ye anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala kuwa, Kamati itakutana Ofisi Ndogo ya Bunge Dar es Salaam, kuanzia tarehe 21, saa tatu asubuhi. Hawa wanakutana Dar es Salaam tarehe 21.

Mwenyekiti wa Kamati ya Masuala ya UKIMWI, Mheshimiwa Lediana Mng'ong'o, ye ye anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati ya Masuala ya UKIMWI kuwa, leo kutakuwa na kikao mara baada ya kipindi cha maswali Bungeni katika Ukumbi Namba 219. Naona kuna wengine Ukumbi Namba 219, nadhani mtakwenda kuelewana huko huko au Makatibu wenu wajue kwamba hapa mme gongana.

Mwenyekiti wa Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge, Mheshimiwa Brig. Gen. Mstaafu Hassan Ngwilizi, anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati hiyo kuwa, leo kutakuwa na kikao mara baada ya kipindi cha maswali Bungeni na kuahirishwa Bunge katika Chumba Namba 231. Kwa hiyo, mnaombwa kuhudhuria huko.

Tangazo hili ni kwa Wabunge wote, tunajiandaa kufanya zoezi la kupiga picha (*passport size*), kwa ajili ya vitambulisho; zoezi linaendelea katika Ukumbi Namba 131, Ghorofa ya Kwanza, Jengo la Utawala. Vitambulisho hivyo vitatumika kupita milangoni na vizuizi vinginevyo. Sasa usipopiga picha, utafika mahali mlango utakataa kufunguka. Kwa hiyo, jitahidini mkapate vitambulisho hivyo, mtakuwa navyo mkipita mlangoni kama ni wahusika basi utafunguka. Vitambulisho hivi havibadiliki. Vitambulisho tulivyonavyo Waheshimiwa Wabunge, iwapo Mbunge hatapiga picha hawezi kupata kitambulisho na litakuwa tatizo kwake katika *access point* kwenye mageti; kwa hiyo, tunaomba na kushauri mshiriki zoezi hili kabla hamjaondoka maana unaweza kufika getini, geti likakukataa. Kwa hiyo, kila Mbunge ajitahidi kupiga hizo picha. Nimesema Chumba Namba 131. Nafikiri wengine walianza, kwa hiyo, nawakumbusha na wengine waliobakia, Ukumbi Namba 131, kabla hamjakwenda nyumbani basi m jitahidi kufanya hivyo.

Wapo Wabunge wengi wanaendelea kuulizia hela za mkopo wa magari wanaona kama hazijaingia kwenye akaunti zao. Zoezi linafanyika wiki hii. Huu ni mkopo; Wananchi mjue huu ni mkopo ambao kila Mbunge na ni mila na desturi za Mabunge yote, Wabunge wakishachaguliwa, wanapewa mkopo wa magari na wanalipa. Siyo jambo la ajabu ni kwamba, siyo Mbunge, nilikuwa nikitoa mfano katika Gazeti moja; Jimbo kama la kwangu, lenye milima na mabonde; hivi kweli unaweza kwenda kwa *Bajaj* au unaweza kutumia Baiskeli? Kwa hiyo, nyenzo mojawapo muhimu ya Mbunge kufanya kazi ni pamoja na matumizi ya gari. (*Makofi*)

Bahati nzuri magari tuliyoyachukua ni yale ya Mkonga, ambayo yanaweza kuhimili aina zote za barabara. Kwa hiyo, hivyo ndivyo ilivyo. Hilo ni deni, siyo kwamba wamepewa bure. Ninaomba ieleweke hivyo kwa Wananchi; ni kwamba, Mbunge wako akitaka kufanya kazi, ni sharti akufikie, kama hawezi kukufikia, basi huyo Mbunge hawezi kufanya kazi yake inavyostahili. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, zoezi hilo linaendelea kuhakikiwa na wiki ijayo nadhani litakuwa limekamilika.

Mwenyekiti wa Kamati ya Miundombinu, ameleta sasa hivi kibarua chake hapa anasema, Kamati ya Miundombinu nao wakutane Dar es Salaam, kuanzia tarehe 21 Februari, kwa ajili ya kujadili mambo ama kujifunza mambo ya Reli, ATCL na

msongamano wa magari; ni kujifunza kwanza, hamuwezi kujadili kitu ambacho hamjajifunza.

Kuna Kikao cha *APNAC*; Sekretarieti ya *APNAC*, inaomba kuwatangazia Wajumbe wote wa Mtandao wa Bunge wa Afrika Wanaopambana na Rushwa (*APNAC*), kuwa leo saa 7.00 mchana kutakuwa na Kikao cha Wanachama wote wa *APNAC* katika Ukumbi wa Msekwa na Waheshimiwa Wabunge wanaotaka kujiunga na Chama hiki pia wanakaribishwa. Ninaona kama Kamati ya Maendeleo ya Jamii pia inakaa huko huko; kwa hiyo, mtajadiliana wenyewe wapi mkakae.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya matangazo hayo, mimi sina matangazo mengine, nadhani tufuate ratiba ilivyo, isipokuwa kama nilivyosema, shughuli zetu zinaishia leo asubuhi hii. Kwa hiyo, tutamwomba Mheshimiwa Waziri Mkuu, aweze kuahirisha Kikao cha Bunge.

**ND. JOHN JOEL – KAIMU KATIBU WA BUNGE:** Mheshimiwa Spika, naomba kutoa taarifa kwamba, shughuli zilizopangwa kwenye Mkutano huu wa Pili wa Bunge, ulioanza tarehe 9 Februari, 2011 kwa sasa zimekamilika.

## KUAHIRISHA BUNGE

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, ni jambo la kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa Rehema, kwa kutupa uhai hadi leo na kutuwezesha kuhitimisha Mkutano huu wa Pili salama.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyotoa Taarifa jana, Taifa letu liko kwenye majonzi na masikitiko makubwa kufuatia Maafa yaliyosababishwa na milipuko ya Mabomu kwenye Maghala ya Kambi ya Jeshi, eneo la Gongo la Mboto, Dar es Salaam. Taarifa zilizopatikana hadi jana jioni zinaonesha kuwa, jumla ya Watu waliopoteza maisha ni 20, majeruhi ni 315 na ambao bado wamelazwa hospitalini ni 135, kwa maana kwamba wengine wameshakuwa *discharged*. Mbali na Maafa ya Vifo na Majeruhi, milipuko hiyo imesababisha hasara kubwa ya mali kwa Wananchi na Taifa kwa ujumla.

Mheshimiwa Rais, jana tarehe 17 Februari 2011, alitembelea eneo la maafa na kujionea uharibifu mkubwa uliotokea. Baada ya kutembelea eneo hilo, Mheshimiwa Rais aliitisha Kikao cha Dharura cha Baraza la Usalama la Taifa ili kutathmini hasara iliyotokea na kubainisha njia za haraka za kuchukuliwa ili kuwasaidia Wananchi wote walioathirika na Maafa hayo. Kama alivyosema Mheshimiwa Rais, tunaomba Wananchi wote wawe watulivu na warejee kwenye maeneo yao wakati Serikali inashughulikia tatizo hilo. Maafa haya yamesababisha mihangainko mionganoni mwa Watanzania. Maafa haya ni yetu sote Watanzania. Waliopoteza maisha na mali zao ni Ndugu zetu. Hivyo, nawaomba Watanzania wote ndani na nje ya Nchi, popote walipo na Washirika wetu wa maendeleo, kuisaidia Serikali kukabiliana na tatizo hili. Nawasihi tushirikiane kuwafariji Waathirika kwa kuwapa misaada mbalimbali ya hali na mali ili waweze kurudia maisha yao ya kawaida mapema iwezekanavyo.

Mheshimiwa Spika, nataka nichukue nafasi hii kukushukuru wewe lakini kuwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge, kwa uamuzi wa dhati mlioufanya leo hii asubuhi, kuchangia posho ya siku moja kwa ajili ya kuwasaidia waathirika wa mabomu. Nawashukuruni sana sana na Mungu awabariki sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, napenda kwa mara nyingine tena, kuwapa pole wote waliokumbwa na maafa haya. Kwa majeruhi wote, nawaombea kwa Mwenyezi Mungu, awajalie nafuu na kupona haraka na kwa wale waliopoteza maisha, tuungane sote kumlilia Mwenyezi Mungu ili azipokee roho zao peponi na kuzilaza Mahala Pema. Amina.

Mheshimiwa Spika, Baraza lilipokutana jana, lilifanya maamuzi ya msingi ambayo baadae yatatolewa ufanuzi na Serikali kuhusu namna tutakavyowahudumia majeruhi, lakini vilevile wale waliopoteza maisha. Lakini pia maamuzi hayo yamezingatia nini kifanyike kuhusu mali za watu wote ambao wamepatwa na matatizo ya kubomolewa nyumba zao. Kwa hiyo, taarifa kamili itatolewa.

Mheshimiwa Spika, leo tunahitimisha shughuli za Mkutano wa Pili wa Bunge lako Tukufu ambao ulianza tarehe 8 Februari 2011. Mkutano huu ndiyo Mkutano wa Kwanza wa Kazi wa Bunge hili, baada ya kukamilisha mchakato wa Uchaguzi Mkuu, ambao ndiyo umetupatia kibali cha kuwa Wabunge wa Bunge la Kumi la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Vilevile, Mkutano huu umefanyika baada ya Semina Elekezi kuhusu Wajibu wetu kama Wabunge, iliyofanyika Dar es Salaam kwa muda wa siku kumi na kufungwa tarehe 3 Februari 2011. Sote tuliohatika kuhudhuria Semina ile, tunakubaliana kwamba, Semina Elekezi ilitujengea uelewa mpana wa masuala ya utendaji, yakiwemo masuala yanayogusa Mihimili mitatu, yaani Mahakama, Bunge na Serikali.

Napenda nitumie fursa hii, kwanza, kuishukuru tena Ofisi yako Mheshimiwa Spika, kwa kuandaa Semina hiyo. Pili, kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote, ambao walishiriki kikamilifu kwa muda wote. Ni dhahiri kwamba, Semina ile imekuwa chachu katika kujipanga kutekeleza majukumu yetu kama Wabunge. Tumepewa fursa, tumejua wajibu wetu, tumebaini changamoto na tumeweka mikakati ya kuzikabili changamoto hizo. Kilichobaki sasa ni kufanya kazi kwa misingi ya maelekezo tuliyoyapata kwa bidii zaidi ili kuongeza tija na ufanisi katika kuwatumikia Wananchi waliotuchagua.

Mheshimiwa Spika, katika Mkutano huu, Ajenda iliyochukua nafasi kubwa ni Hoja ya Serikali ya Kujadili Hotuba ya Mheshimiwa Rais. Hoja hiyo tumeihitimisha vizuri na kwa mafanikio makubwa. Napenda kuwapongeza tena Waheshimiwa Wabunge wote, kwa kushiriki katika mjadala wa Hotuba hiyo vizuri. (*Makofi*)

Vilevile, katika Mkutano huu, tumeweza kufanya Chaguzi za Wenyeviti na Makamu Wenyeviti wa Kamati za Kudumu za Bunge. Vilevile, tulifanya chaguzi za Wajumbe wa kutuwakilisha katika Kamati na Taasisi mbalimbali za Kitaifa na Kimataifa.

Kwa vile orodha ni ndefu, napenda nitumie nafasi hii, kuwapongeza kwa dhati kabisa na kwa ujumla wao, wote waliogombea nafasi hizo na kushinda. Ni matarajio yangu kwamba, tutatumia nafasi hizo vizuri katika kuleta ushirikiano, mshikamano na kufanya kazi kwa pamoja kama Wawakilishi wa Wananchi wa Tanzania na kutekeleza majukumu yetu kama Wabunge ndani ya Bunge hili.

Mheshimiwa Spika, katika Mkutano huu wa Pili wa Bunge, jumla ya Maswali 95 ya Msingi na Maswali 187 ya Nyongeza yaliulizwa na Waheshimiwa Wabunge. Vilevile, utaratibu wa Maswali kwa Waziri Mkuu kila Alhamisi uliendelea kwa Waheshimiwa Wabunge kuuliza Maswali matano ya Msingi na manne ya Nyongeza.

Mheshimiwa Spika, katika Mkutano huu pia Miswada ya Serikali ifuatayo ilisomwa kwa mara ya kwanza:-

- i) Muswada wa Sheria ya Manunuzi ya Umma wa Mwaka 2010 (*The Public Procurement Bill, 2010*);
- ii) Muswada wa Sheria ya Famasia wa Mwaka 2010 (*The Pharmacy Bill, 2010*);
- iii) Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali wa Mwaka 2011 (*The Written Laws (Miscellaneous Amendments) Bill, 2011*); na
- iv) Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria za Maeneo ya Maendeleo ya Kiuchumi wa Mwaka 2011 (*The Economic Zones Laws (Miscellaneous Amendments) Bill, 2011*).

Mheshimiwa Spika, Bunge lako Tukufu lilipokea Kauli ya Serikali kuhusu Uamuvi wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, inayohusu Kuanzisha Mchakato wa Kuitazama Upya Katiba ya Nchi kwa Lengo la Kuihuisha ili Kuendana na Mabadiliko na Matakwa na Hali ya Sasa na Baadaye. Aidha, Bunge lako Tukufu lilipokea Kauli za Serikali Kuhusu Utekelezaji wa Programu ya Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini na ile ya Hali ya Umeme Nchini na Utekelezaji wa Miradi ya Umeme Katika Kipindi Kifupi na cha Kati.

Mheshimiwa Spika, siku mbili zilizopita, tarehe 15 Februari 2011, nilisimama hapa kutoa maelezo na ufanuzi wa hoja na masuala mbalimbali yaliyotokana na majadiliano ya Hotuba ya Mheshimiwa Rais ya kuzindua Bunge la Kumi. Kwenye maelezo yangu, nilizungumzia mambo mbalimbali yakiwemo marekebisho ya Katiba ya Zanzibar, Masuala ya Muungano, Umoja wa Kitaifa, Sekta za Kijamii, hali ya Uchumi na Migomo na Maandamano kwenye Vyuo Vikuu.

Kabla ya kutoa maelezo na ufanuzi wangu, nilitanguliwa na Mawaziri tisa waliojibu hoja mbalimbali za Waheshimiwa Wabunge kwenye Sekta zao. Aidha, kabla ya Waheshimiwa Mawaziri kujibu hoja hizo, Serikali ilikuwa imeshatoa Kauli kwenye Masuala ya Kurekebisha Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Maji na Nishati.

Ninaamini, kwa maoni yangu, maelezo na ufanuzi wangu, Kauli za Serikali na majibu ya Waheshimiwa Mawaziri, yalionesha dhahiri wapi tunatoka, wapi tulipo na wapi tunaeleke. Safari bado ni ndefu, lakini kwa kushirikiana na kuweka Itikadi zetu za Kisiasa pembeni na kutanguliza mbele mahitaji na matatizo ya waliochagua na kutuleta ndani ya Jengo hili tutafika, tena tutafika salama. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kabla ya kuhitimisha maelezo yangu, napenda kuwaeleza Waheshimiwa Wabunge na Wananchi kwamba, hali ya Chakula imeendelea kuwa nzuri katika maeneo mengi Nchini kwa kipindi cha mwaka 2010/2011, kufuatia mavuno mazuri ya mwaka 2009/2010. Tathmini iliyofanyika mwezi Desemba 2010 ilionesha kwamba, uzalishaji wa mazao ya chakula katika msimu wa 2009/2010 ulifikia Tani Milioni 12.3 zikiwemo Tani Milioni 7.4 za mazao ya nafaka na Tani Milioni 4.9 za mazao yasiyo nafaka. Mahitaji ya Chakula kwa mwaka 2010/2011 ni Tani Milioni 11.1; hivyo, uzalishaji huu utatosheleza mahitaji ya Chakula kwa Asilimia 111, sawa na ziada ya takriban Tani Milioni 1.2. Baadhi ya maeneo ya Nchi yalipata mavuno ya ziada na mengine kujitosheleza. Kufuatia hali hiyo, upatikanaji wa Chakula katika maeneo mengi ya Nchi, hususan katika Masoko ya Vijijini na Mijini bado umekuwa ni wa kuridhisha.

Hadi tarehe 14 Februari 2011, Akiba ya Chakula katika Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula (*NFRA*) ilikuwa jumla ya Tani 216,030.653 za mahindi ambazo ziko katika Kanda mbalimbali za Hifadhi ya Chakula ya Taifa. Aidha, kiasi cha Tani 176,083 za mazao ya nafaka zilikuwa kwa Wafanyabiashara Binafsi.

Hata hivyo, kama nilivyoliezea Bunge lako Tukufu, yako baadhi ya maeneo ambayo yameonesha dalili ya kuwa na upungufu wa chakula kati ya mwezi Januari na mwezi Machi 2011. Maeneo hayo ni yale yanayopata mvua za vuli na ambako mvua hizo hazikunyesha vizuri. Tayari Serikali imeanza kuchukua hatua kwa kutenga jumla ya tani 13,760 za chakula kutoka Hifadhi ya Taifa kwa ajili ya Watu 423,530 ambao wameainishwa kwamba, wanakabiliwa na upungufu wa chakula. Aidha, Serikali itafanya uchunguzi mwingine hivi karibuni ili kuweza kubaini maeneo mapya ambayo nayo yataingizwa katika utaratibu huo yatakapoabitika kwamba yana tatizo kubwa la uhaba wa chakula.

Nitumie fursa hii kutoa wito kwa Wananchi wote kutumia chakula kilichopo kwa uangalifu kama njia mojawapo ya kujihami na Janga la Njaa linaloweza kutokea. Aidha, kila mmoja wetu anao wajibu wa kuchukua tahadhari mapema. Nawaomba Waheshimiwa Wabunge, tunaporudi Majimboni mwetu, tutumie muda huo kuwaasa Wananchi, hasa wale wenyewe mavuno machache, umuhimu wa kutunza chakula. Vilevile, Wakulima wahimizwe kutumia mvua zinazonesha kupanda mazao yanayoendana na hali ya hewa ya maeneo yao. Upande wa Serikali tutajitahidi kuona kama tunaweza kuona kama tunaweza kupata mbegu ya ziada inayoweza kutumika katika kipindi hiki mvua zinapoanza kunyesha.

Mheshimiwa Spika, katika muda mfupi tuliokaa pamoja hapa Bungeni, nimegundua kuwa, tuna Waheshimiwa Wabunge mahiri waliobobea katika nyanja mbalimbali. Wapo wasomi wa ngazi zote; Wazee kwa Vijana, ambao wana uzoefu na

utaalam mkubwa. Ni imani yangu kuwa, tutatumia Utaalam, Umahiri na Uwezo wetu mkubwa tulionao katika kuijenga Nchi yetu na kuwasaidia Watanzania kutoka hapa tulipo hadi hatua ya mbele katika kuleta maendeleo ya Nchi yetu. Wananchi walio tuchagua wanatutegemea sana. Nawaomba tutangulize Uzalendo katika kila jambo tufanyalo, kwa manufaa ya Taifa letu na Watu wake, badala ya ushabiki wa Kisiasa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, napenda kuhitimisha Hotuba yangu kwa kurejea tena kusema kwamba, baada ya kukamilika kwa Uchaguzi Mkuu kwa mafanikio makubwa, kazi kubwa iliyo mbele yetu ni kuijenga Nchi yetu kwa Umoja na Mshikamano mkubwa. Nawaomba tuweke maslahi ya Watanzania na Taifa mbele. Tudumishe Amani na Utulivu. Tupuuze Sera zozote za kudhoofisha Utaifa wetu kama Watanzania na kutugawa kwa misingi yoyote ile, iwe ya Kikabila, Imani za Dini, Rangi au kwa Itikadi za Kisiasa. Dhamira yetu sote iwe ni kukuza uchumi wa Nchi yetu na kuondoa umaskini ili kuwa letea Wananchi wetu maendeleo na maisha mazuri. Ni jukumu la kila mmoja wetu kuhakikisha kuwa, Tanzania inapiga hatua mbele. Tufanye kazi kwa bidii, juhudii, maarifa na ubunifu zaidi. Mimi naamini kuwa, kwa ushirikiano wa Bunge hili na Wananchi kwa ujumla, tutaweza kutimiza matarajio ya Wananchi walio tuchagua na matarajio ya Watanzania wote.

Mheshimiwa Spika, mwisho, nawashukuru wote waliofanikisha Mkutano huu wa Pili wa Bunge. Shukrani za pekee ni kwako wewe Mheshimiwa Spika, kwa kudhihirisha kwamba una uwezo mkubwa wa katuongoza ndani ya Bunge hili. Ni dhahiri umeanza vizuri, tunakupongeza kwa dhati kabisa. Namshukuru vilevile, Naibu Spika, kwa umahiri wake wakati wa kuongoza Vikao vya Bunge hili. (*Makofi*)

Nawashukuru pia Waheshimiwa Wabunge, kwa michango yenu ambayo japo kwa wengine ilikuwa mara ya kwanza kuchangia hapa Bungeni, wote mmeonekana Wazoefu wa siku nyingi katika kuchangia hoja zilizowasilishwa kwenye Mkutano huu. (*Makofi*)

Namshukuru Katibu wa Bunge, Dkt. Thomas Kashilillah na Wasaidizi wake, kwa huduma mbalimbali ambazo zilifanikisha Mkutano huu. Nawashukuru Watumishi wa Serikali, Taasisi mbalimbali na Waandishi wa Vyombo mbalimbali vyta Habari, kwa kutoa taarifa za mambo yote yaliyojadiliwa katika Mkutano huu kwa wakati. Wote kwa ujumla wao, nawashukuru sana.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, nawatachia wote safari njema. Naomba kutoa hoja kwamba, Bunge lako Tukufu sasa liahirishwe hadi Siku ya Jumanne, tarehe 5 Aprili, 2011, Saa Tatu Asubuhi, litakapokutana katika Mkutano wa Tatu hapa Mjini Dodoma.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

**WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

**SPIKA:** Nawashukuru maana wote mmeunga mkono hoja ya Serikali. (*Kicheko*)

Waheshimiwa Wabunge, kabla sijawahoji mimi pia ninapenda kutoa shukrani zangu za pekee kwamba, hili lilikuwa Bunge letu la Kwanza na mimi ukiniambia nifanye tathmini bila kukaa kwenye Kamati yangu ya Uongozi, tumefanya kazi vizuri sana. Mmefanya kazi vizuri sana, mmejitahidi kuzielewa Kanuni; mnapofanya changamoto kwa Spika, ninyi hamjui tu, mnamuimarisha Spika zaidi; maana kama alikuwa hajui Kanuni anatafuta sasa inaingia kichwani na inabaki huko huko. Ukiwa na changamoto unajifunza zaidi kuliko kama ungekuwa huna changamoto. (*Makofi/Kicheko*)

Waheshimiwa Wabunge, napenda ieleteke kwamba, tukiwa katika Bunge jamani sisi ni wamoja, yaani hata ukifanya vituko vyako vile wewe uko ndani ya Bunge tuko pamoja tu. Kwa hiyo, isionekane kama upande wetu umefanya vituko basi ikaonekana ni tatizo la Spika na Mbunge; si kweli. Mimi hapa nitawaongoza kwa mujibu wa Kanuni. Sasa naweza kukwambia ufanye hivi na si kwamba wewe ni adui yangu; wewe si adui yangu. Mimi nikimaliza hapa nimeondoka, kwa hiyo, usije ukaweka roho yako ikawa na kifundo cha aina fulani kwamba Spika alifanya hivi utaumia bure.

Spika kwa mujibu wa Kanuni ya Nane ni Spika wa Bunge; siyo Spika wa CCM au wa chama chochote. Kanuni zetu zitachapa pande zote. Kwa hiyo, mimi naomba muwe na furaha, tufanye kazi zetu kwa furaha, yaani kila mtu ajisikie anataka kurudi Bungeni. Kama una vituko vyako unataka kuvileta, lete hapa tu hakuna tatizo ndiyo utaratibu kwa mujibu wa Kanuni. Kwa hiyo, tunapofanya kazi hapa hatuna uadui, hata mwenzio akikwambia neno ambalo limekuudhi ukubali kwamba anacheza mchezo wa hapa hapa tu, mkitoka nje nendeni mkanywe chai vizuri, mkashikane mikono na endeleeni na kazi. (*Makofi*)

Kwa hiyo, mkifanya hivyo mtakuta tunafanya kazi nzuri na Wananchi wanaotuangalia hapa, maana tunaonekana *live* hapa, wanatuona kwamba watu wanafanya kazi yao; lakini mkiondoka hapa na vinyongo au mkienda huko mnaanza kutoa maneno mengine nje ya hapo si utaratibu. Halafu nimezuia kutumia Kanuni; kuna watu wanatoka humu wanakwenda kutoa maneno nje, ile Kamati yetu ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge inaweza kufanya kazi yake, lakini ni kwa sababu tulielewa kwamba bado tunaendelea kujifunza; naomba hili mlielewe. Wewe kama una shida yako sema hapa, kama hukuridhika na mtu yejote kuna Kanuni ziko nyingi hapa. Baada ya kuahirisha Bunge unasema maneno yako yote na hasira zako humu humu ndani halafu tunamaliza tunaendelea. Kwa hiyo, hilo ndiyo nilifikiri tujifunze kwamba, muwe huru. Hivi si viwanja vyaa siasa kama kule mnakopambana, humu ni Bunge ndiyo maana tuko *secular*. Maana kama ya zamani unakuta unakaa upande kabisa, *strict* hivi, lakini sisi tuko *secular* na Spika anakaa katikati kwa maana sisi tupo pamoja. (*Makofi*)

Kwa hiyo, hilo nadhani tutajifunza vizuri zaidi katika Bunge linalofuata na tutaendelea kujifunza hivyo na mimi ninachotaka ni *freedom* ya Wabunge, uwezo wa kuuliza na kudadisi humu ndani. Tutaendelea kuongozana na Kanuni zetu zile nadhani kipindi hiki Kamati ya Kanuni itapewa mapendekezo tuliyokuwa tumeyaleta ya kufanya mabadiliko katika maeneo fulani. Tuliacha kusudi Wabunge muanze kuzoeazoea hivi kwa sababu mnaweza kushiriki pia kwamba labda tungeongeza mabadiliko fulani katika Kanuni. Ndiyo maana tulichelewesha kidogo kusudi mpate nafasi ya uzoefu kidogo, tutakopokuja kubadilisha na ninyi mnayo sababu ya kushiriki katika mabadiliko yanayofuata.

Baada ya kusema hivyo, napenda kusema kwamba, tutaahirisha Kikao cha Bunge mpaka tarehe 5 Aprili, 2011, lakini wakati huo huo tunatanguliwa na Wimbo wa Taifa halafu nitawahoji baadaye. Naomba tusimame kwa ajili ya Wimbo wa Taifa.

## **WIMBO WA TAIFA**

*(Hapa Wabunge Waliimba Wimbo wa Taifa)*

**SPIKA:** Tukae. Waheshimiwa Wabunge, sasa nitawahoji kwamba Bunge sasa liahirishwe mpaka tarehe 5 Aprili, 2011.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)  
(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**SPIKA:** Mmenogewa na Dodoma! Walioafiki wameshinda; kwa hiyo, Bunge linaahirishwa mpaka tarehe 5 Aprili, 2011.

*(Saa 5.15 asubuhi Bunge liliahirishwa mpaka Siku ya Jumanne,  
Tarehe 5 Aprili, 2011 Saa Tatu Asubuhi)*